# UTOHOZI WA MSAMIATI KUTOKA KISWAHILI HADI EKEGUSII

EMILY KEMUNTO MOSOTA

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library
0547900 1

2016

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi.................................................................. Tarehe 20th Sep 2016

**Emily Kemunto Mosota**

**C50/66993/2013**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi.................................................................. Tarehe 07/11/2016

**Dkt. Nyachae Michira**

Sahihi.................................................................. .Tarehe 20.09.2016

**Dkt. Hanah Mwaliwa**

**TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa: Wazazi wangu Richard Mosota Ogesare na mama Lucy Bwari kwa kunipa moyo kila wakati wa kuendelea na masomo yangu. Wanangu wapendwa Belden, Velma na Theophilus.

# SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kuendeleza masomo yangu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu, Daktari Nyachae Michira na Daktari Hannah Mwaliwa kwa kuniongoza, kunielekeza na kuihakiki kazi yangu.

Nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili chuo cha Nairobi kwa kujitolea kwa hali na mali kunifunza, kazi yao nzuri ilinisaidia kwingi. Hasa mchango wa Iribe Mwangi katika uteuzi wa mada yangu si haba. Mungu awabariki. Nawatolea shukrani wanafunzi wenzangu wa uzamili kwa ushirikiano wenu kwa muda tuliosoma pamoja.

Nachukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa mume wangu Elijah Nyabuga kwa kunivumilia na kunihimiza wakati wote nikisoma na kuandika kazi hii. Pia nawashukuru wanangu Belden, Velma na Theophilus kwa kuvumilia sana nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Shukrani za kipekee kwa babangu Richard Mosota, baba ndiye nguzo ya maisha yangu. Ndugu yangu James kwa kunipa moyo kila wakati na ndugu zangu wote.

Kadhalika sina budi kuwatolea shukrani zangu za dhati walimu watajwa kwa mchango wao, mwalimu mkuu Bwana Evans Obiri kwa kunipa ruhusa kila nilipohitajika kwa shughuli hii, Ezekiel ombaso otwere, Thomas Moracha Makwabe, mwalimu Yobesh Anyona na Vitalis Achira. Mchango wao wote ulinifaa mno. Aidha sitamsahau bwana Yobesh Mogire aliyenipa moyo wa kuendelea na tasnifu hii.

Kufanikiwa kwangu katika kuhitimisha kazi hii kumetokana na juhudi za watu wengi lakini kwa sababu ya kubanwa na wakati na nafasi, sitaweza kuwataja wote. Kwa hivyo, ningependa kuwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kwa kuwa msaada wenu ulinifaa sana, Mungu awabariki nyote.

# Ikisiri

Utafiti huu una lengo la kuweka wazi usayansi uliopo katika istilahi zilizotoholewa kutoka Kiswahili hadi Ekegusii. Utafiti huu umetumia nadharia ya ukopaji uhamisho na N.I.K. katika ufafanuzi wa kazi hii. Vile vile uasilia wa istilahi tohozi umechunguzwa iwapo maneno tohozi yote yalikuwa na majina asilia. Tumegundua kuwa majina asilia mengi yanazidi kufifia kwa kuwa watumizi wa nomino hizo ni wachache. Mofolojia ya Kiswahili na ya Ekegusii imelinganishwa. Ukosefu wa fonimu fulani katika lugha moja ndio husababisha tofauti katika maendelezi. Tofauti kati ya lugha hizi mbili ulibainishwa ingawa zote ni lugha za nasaba moja. Taratibu za utohozi zimechunguzwa, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa utohozi huongozwa na kudhibitiwa na sheria na kanuni za fonolojia ya Ekegusii.

## ISHARA NA AKRONIMU ZILIZOTUMIKA

| | |
|---|---|
| ( ) | mabano ya kijumla |
| [ ] | mabano ya fonetiki |
| / / | mabano ya fonimu |
| **I** | irabu |
| **Kons** | konsonanti |
| **NIK** | Nadharia ya Istilahi ya Sayansi |
| **UMK** | sheria ya Ugeuza Maumbo Kidhana |
| **PEGITOSCA** | Vifupisho Vinavyounda Akronimu |
| **P** precision | udhahiri |
| **E** economy | iktisadi |
| **G** generativity | uzalishaji |
| **I** internationality | umataifa |
| **T** transparency | uangavu |
| **O** non- obscenity | utusani |
| **S** systemicity | utaratibu maalum |
| **C** consistence | utaratibu ulio sawa |
| **A** appropriateness | ukubalifu/ufaafu |

## YALIYOMO


**UNGAMO** ........ ii

**TABARUKU** ........ iii

**SHUKRANI** ........ iv

**IKISIRI** ........ v

**ISHARA NA AKRONIMU ZILIZOTUMIKA** ........ vi

**YALIYOMO** ........ vii

**UTANGULIZI** ........ 1

1.1 Lugha Zinazoshughulikiwa ........ 2

1.1.1 Ekegusii ........ 2

1.1.2 Kiswahili ........ 3

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.3 Malengo Ya Utafiti ........ 4

1.4 Nadharia tete ........ 4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 5

1.6 Upeo na Mipaka ........ 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 6

1.7.1 Dhana ya ukopaji ........ 7

1.7.2 Dhana ya utohozi ........ 8

1.8 Msingi wa Kinadharia ........ 10

1.8.1 Nadharia ya Ukopaji Uhamisho ........ 10

1.8.2 Nadharia ya Istilahi ya Kisayansi (NIK) ........ 12

1.9 Mbinu Za Utafiti ........ 15

1.1 0 Kukusanya Data ........ 16

1.11 Kuchanganua Data ........ 16

**SURA YA PILI: UASILIA WA MSAMIATI ... 18**
2.1 Utangulizi ... 18
2.2 Sayansi na teknolojia ... 18
2.3 Isitlahi za kimasomo ... 19
2.4 Msamiati wa jikoni ... 20
2.5 Msamiati wa mavazi na mapambo ... 21
2.6 Msamiati wa dini ... 23
2.7 Msamiati wa wanyama ... 24
2.8 Msamiati wa vyakula ... 25
2.9 Siku za wiki ... 25
2.10 Majira na nyakati ... 26
2.11 Sehemu za Mwili ... 27
2.12 Hisabati ... 28
2.13 Nominoambata ... 29
2.15 Hitimisho ... 30
**SURA YA TATU: MOFOFONOLOJIA YA EKEGUSII ... 31**
3.1 Utangulizi ... 31
3.2 Vokali za Ekegusii ... 32
3.3 Sehemu ya Kutamkia Vokali ya Ekegusii ... 34
3.4 Konsonanti za Ekegusii ... 34
3.5 Vokali za Kiswahili ... 38
3.6 Hitimisho ... 40
**SURA YA NNE: TARATIBU ZA UTOHOZI FONOLOJIA ... 41**
4.1 Utangulizi ... 41
4.2 Dhana ya istilahi ... 41
4.3 Maana ya msamiati wa Ekegusii ... 42

4.4 Isimu ........................................................ 42

4.5 Maana ya usayansi ........................................................ 42

4.6 Utohozi Fonimu ........................................................ 43

4.7 Utohozi wa Konsonanti ........................................................ 43

4.8 Utohozi vokali ........................................................ 49

4.9 Mofolojia ya Ekegusii ........................................................ 51

4.9.1 Uambishaji ........................................................ 52

4.9.2 Uambatishaji ........................................................ 55

4.10 Hitimisho ........................................................ 56

**SURA YA TANO: HITIMISHO ........................................................ 58**

5.1 Utangulizi ........................................................ 58

5.2 Muhtasari wa Matokeo ........................................................ 58

5.3 Mapendekezo ya Utafiti ........................................................ 59

5.4 Hitimisho ........................................................ 60

**MAREJELEO ........................................................ 61**

**KIAMBATISHO. ........................................................ i**

# ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali: 2:1 Sayansi na teknolojia ........ 18

Jedwali 2.2 Isitlahi za kimasomo ........ 19

Jedwali 2.3 Msamiati wa jikoni ........ 21

Jedwali 2.4 Msamiati wa mavazi na mapambo ........ 22

Jedwali 2.5 Msamiati wa dini ........ 23

Jedwali 2.5.1 Utohozi Tafsiri ........ 24

Jedwali 2.6 Msamiati wa wanyama ........ 24

Jedwali 2.7 Msamiati wa vyakula ........ 25

Jedwali 2.8 Siku za wiki ........ 26

Jedwali 2.10 Sehemu za mwili ........ 27

Jedwali 2.10.1 Sehemu za mwili zilizotoholewa ........ 28

Jedwali 2.11 Hisabati ........ 28

Jedwali 2.12 Nomino ambatano ........ 29

Jedwali 3.1Vokali za Ekegusii ........ 33

Jedwali 3.2 Vokali ya Ekegusii ........ 34

Jedwali 3.3 Konsonanti za Ekegusii ........ 35

Jedwali 3.4 Wingi wa nomino ........ 36

Jedwali 3.5 Sehemu za kutamukia konsonanti za Ekegusii ........ 37

Jedwali 3.6 Matumizi ya Fonimu /j/ ........ 37

Jedwali 3.7 Vokali za Kiswahili ........ 38

Jedwali 3.8 Konsonanti za lugha ya kiswahihili ........ 39

Jedwali 4.1 Nomino zilizochopekwa vokali ‘a’ ........ 52

Jedwali 4.1.1 Udogo ........ 53

Jedwali 4.2 Nomino zinazochopekwa vokali ‘o’ ........ 53

Jedwali 4.3nomino zinazochopekwa vokali ‘e’ ........ 54

Jedwali 4.4 Nomino ambata ........ 56

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Watu wanaozungumza lugha mbili au zaidi wanapotagusana kuna uwezekano wa uwiano wa utamaduni. Baadhi ya matokeo ya mtagusano huo ni ukopaji, utohozi, uwili lugha, ulumbi lugha, kuchanganya ndimi, pijini, krioli na lugha mfu. Utafiti wetu utaangazia maneno tohozi kutoka Kiswahili ambayo ni lugha chanzi hadi Ekegusii ambayo ni lugha pokezi. Maneno tohozi mengi yametoholewa ili kukubaliana na muundo wa lugha kopaji.

Baadhi ya mambo ambayo huchochea utohozi wa msamiati ni ukosefu wa msamiati wa kutajia dhana au jambo fulani, maendeleo ya kiteknolojia, kutofautisha mawazo mawili yanayokaribiana na yaliyo na utata, nia ya kutaka kutumia maneno machache na pia kujitambulisha na hadhi fulani.

Utohozi hutokea katika viwango vyote vya lugha ambavyo ni fonolojia, mofolojia sintaksia, semantiki na pragmatiki. Kuna aina tatu za ukopaji, ukopaji wa moja kwa moja ambao ndio sisisi, maneno hunukuliwa yalivyo na kutumika vivyo hivyo, mfano. Majina ya miezi. Utohozi ambao unahitaji maneno kufasiriwa katika lugha kopaji ambao ni utohozi kwa tafsiri. Na utohozi unaohusu kubadilishwa kwa maneno yaliyokopwa kwa kuzingatia viwango vya lugha pokezi.

Utafiti huu unachanganua kimofonolojia nomino tohozi za Ekegusii zinazotokana na Kiswahili.Tutabainisha kanuni zinazoongoza michakato mahususi. Utafiti huu ni mchango muhimu katika taaluma ya isimu linganishi kwa kuwa inahusisha lugha mbili Kiswahili na Ekegusii.Utafiti huu utasaidia katika ufundishaji wa lugha ya pili kwa sababu vikwazo vya kifonolojia vya lugha hizi mbili vimewekwa bayana. Mchango wa utohozi umechangia katika

kuwepo kwa lugha ya Ekegusii kwa kuwa umefanikiwa kupata istilahi za kutumika katika mawasiliano ya kila siku.

## 1.1 Lugha Zinazoshughulikiwa

### 1.1.1 Ekegusii

Wanaozungumza Ekegusii ni Abagusii. Wanaishi katika Gatuzi la Kisii na Nyamira. Abagusii ni Wabantu ambao njia yao kuu ya kujipatia riziki ni kwa ukulima. Wamepakana na Wakipsigis sehemu ya Mashariki, Wamaasai sehemu ya Kusini Mashariki, Wakuria sehemu ya Kusini na Wajaluo sehemu ya Magharibi.

Ochichi (2011) anasema kwamba idadi ya Abagusii ni zaidi ya watu milioni 2.2 ambao ni asilimia kumi ya jumla ya watu nchini Kenya, kuambatana na takwimu za sensa ya 2009. Anasema kuwa asilimia kubwa ya Abagusii ni wana uwili lugha kwa maana kuwa watu wengi wa jamii hii wanazungumza zaidi ya lugha moja. Kulingana na takwimu za SIL (2009) Ekegusii pia huzungumzwa nchini Tanzania katika eneo la Mara na Mkoa wa Serengeti, Mtaa wa Kyambahi Ochichi (2011)

Ekegusii ina lahaja mbili, lahaja ya Kaskazini (*rogoro*) na lahaja ya Kusini *(Maate).* Lahaja hizi mbili zina tofauti chache za kimatamshi. Lahaja ya kusini hutokana na mwingiliano kati ya Abagusii na Wajaluo ambao hutamka /t/ kama /d/. mfano Jina la mtu Otondi wanalitamka kama Odondi. Ulimi wa wanaozungumza lahaja ya Kusini ni mzito kiasi. Kutokana na mwingiliano huu, watu wa kusini huwa na majina tofauti ya kurejelea vitu ingawa wote wanaelewana, mfano: panga, wa kusini wataita *ebeti* na kaskazini wataita *omoro* kishamba kidogo cha mboga ambacho wa kaskazini wanaita *egeticha* wa kusini watakiita *ekerundu.*

### 1.1.2 Kiswahili

Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Inatambulika kuwa lugha ya Kibantu kwa kuwa miundo ya lugha za kibantu ni KI mfano nomino kitabu (*egetabu*), KKI mfano Mungu (Nyasae), KKKI mfano ndwele. Ni lugha ya kitaifa kwani ndio lugha inayotumiwa kuwaunganisha makabila mbalimbali nchini katika shughuli kama vile biashara na dini. Ni lugha rasmi nchini, aidha ni somo rasmi nchini. Kulingana na Iribe Mwangi na Mukhwana (2011) Kiswahili hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa katika shule za msingi na za upili nchini Kenya

Watafiti kama vile Kishe (2002), Ruhumbika (2006) na Livomova (2008) hawajakubaliana kuhusu idadi ya lahaja za Kiswahili. Hata hivyo, wametaja lahaja zifuatazo: Kiunguja, Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kivumba, Kihadimu, Kimtangata, Chichifundi, chi-miini, Ki-siu, Kingwana na Kitumbatu.

Kiswahili sanifu ni lahaja iliyosanifishwa na kiunguja Gromoova (2008). Lahaja hii sanifu ndio lahaja rasmi inayofunzwa na kutahiniwa shuleni, ndiyo inayotumika katika maandishi na katika mikutano rasmi.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Dhana ya utohozi ni muhimu kutazamwa kwani ni mojawapo ya mbinu za uundaji wa istilahi za lugha. Imedhihirika kuwa msamiati wa Ekegusii umetoholewa kutoka kwa Kiswahili. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu dhana hii ya utohozi, wengi wa watafiti wanataja tu kuhusu utohozi, hawaelezi kama maneno haya yaliyotoholewa yalikuwa na majina asilia au la, mfano nomino sahani imetoholewa na kifaa hicho kurejelewa kama *esani* kwa Ekegusii lakini jina lake asilia ni *ekee.*. Mogaka (2009) ameshughulikia dhana ya utohozi wa maneno kutoka Kiswahili hadi Ekegusii, ingawa ametaja kanuni chache za utohozi kifonolojia, hakuzingatia utohozi wa

kimofolojia. Obara (2010) ametafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii, alirejelea makosa ya kifonolojia kama vile uchopekaji wa irabu-u, na udondoshaji wa sauti /h/, aliacha pengo pale ambapo hakueleza kisababishi cha makosa haya. Utafiti wetu utaangazia kinachosababisha mabadiliko haya ya kifonolojia. Ingawa watafiti wa awali wameshughulikia utohozi kifonolojia, kuna pengo kwa kuwa hawajashughulikia utohozi kimofofonolojia. Utafiti huu utaangazia nonimo kama kipashio kuu kinachotoholewa katika lugha ya Ekegusii na kuangazia kanuni kuu zilizo tumika katika utohozi. Tutaangazia kanuni za utohozi kimofofonolojia. Utafiti utafafanua waziwazi na kuonyesha kuwa utohozi huongozwa na kanuni na vigezo vya lugha husika.

## 1.3 Malengo Ya Utafiti

a) Kuchunguza kama nomino zote zilizotoholewa kutoka Kiswahili hadi Ekegusii zilikuwa na majina asilia katika Ekegusii.

b) Kubainisha vigezo vya kimofofonolojia vinavyohusika katika kutohoa maneno kutoka kwa Kiswahili na kuingizwa katika Ekegusii

c) Kuweka wazi kanuni za kimofofonolojia zinazodhibiti utohozi wa nomino kutoka Kiswahili hadi Ekegusii

## 1.4 Nadharia tete

a) Nomino za Ekegusii zilizotoholewa kutoka kwa Kiswahili zilikuwa na majina ya kiasilia yasiyo majina ya utohozi.

b) Utohozi wa nomino za Ekegusii kutoka Kiswahili unazingatia vigezo vya fonimu za lugha husika.

c) Kuna kanuni za kimofofonolojia zinazoongoza utohozi wa nomino kutoka Kiswahili hadi Ekegusii.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Nchini Kenya, Kiswahili ni somo la lazima katika viwango vya shule za msingi na sekondari. Uchunguzi huu wa maneno yaliyotoholewa unaweza kutumiwa katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili shuleni kwa kuonyesha chanzo cha makosa ya kimatamshi. Kwa kushadidia utafiti huu utawasaidia wasomi wanaozungumza lugha ya Ekegusii kuboresha matamshi yao. Lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwa hivyo utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wasomi wa lugha hasa wale wanaozungumza Ekegusii. Tafiti nyingi zilizofanywa kwa mfano Bosire (1993), Mwihaki (1998), Mathooko (2004) na Muadike (2007) zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, tafiti katika lugha ya Kiswahili zinahitajika

Uchunguzi huu utakuwa muhimu kwa wanaisimu wa lugha za wabantu. Data husika itaweza kutumika badala ya kurejelea tahakiki za lugha ya Kiingereza. Utafiti utatumiwa kuweka wazi tofauti zilizoko kwa lugha ya Ekegusii na lugha ya Kiswahili. Hivyo data hii yaweza kutumika katika isimu linganishi. Data hii vilevile yaweza kutumiwa kutafsiri Kiswahili kwa Ekegusii au kutoka Ekegusii kwa Kiswahili.

Kulingana na ruwaza ya Kenya 2030, mbali na kwamba inatambua sera ya taifa ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili kuwa rasmi imeweka pia hamazisho na mkazo katika uendelezaji wa lugha za kiasili nchini Kenya kwa kuhimiza zifanyiwe utafiti wa maswala mbalimbali ya kiisimu, fasihi na utamaduni wa lugha hizi kuwekwa bayana na kufafanuliwa. Utafiti utaweka bayana maswala ya kiisimu ya lugha ya Ekegusii ambapo ni mchango mkubwa katika isimu ya lugha za Kenya na Afrika kwa jumla

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utohozi unaweza kufanywa kwa viwango tofauti, kiwango cha leksia, fonolojia, sintaksia, semantiki au viwango vya tahajia. Hata hivyo, utafiti huu umeangazia utohozi wa maneno pekee. Anavyosema Thomason na Kaufman (1988) katika harakati za ukopaji, elementi ngeni ya kwanza kuingia katika lugha mkopo ni neno. Utafiti huu utajikita katika utohozi wa nomino pekee na wala sio aina nyinginezo. Utangulizi unavyoonyesha, msamiati wa lugha ya Ekegusii umetoholewa kutoka kwa lugha jirani, lakini katika utafiti huu tumeshughulikia nomino zilizotoholewa kutoka asili ya Kiswahili na za Uarabuni. Utohozi unahusu kubadilishwa kwa maneno yaliyotoholewa kwa kuzingatia fonolojia ya lugha pokezi, uchunguzi huu umeegemea utohozi mofofonolojia

Vilevile inabainika kuwa Abagusii wanapatikana katika kaunti ya Nyamira na Kisii. Haikuwezekana kutafiti katika eneo lote hili, utafiti ulijikita katika eneo la Tarafa ya Mosocho. Hii ni kwa sababu tuliweza kupata wazungumzaji asili wa lugha ya Ekegusii ambao hawajaathiriwa pakubwa na lugha nyingine kama Kijaluo, Kiswahili, Kibaluhya, Kimeru na nyingi nyinginezo. Abagusii wanaoishi mijini au mipakani hawakuhusishwa katika utafiti kwa sababu ya kule kutangamana kwao na watu wa lugha nyingine. Athari za lugha hizo zingesababisha kuwepo kwa data isiyo sahihi na isiyoaminika. Lahaja iliyotumika katika kazi hii ni lahaja ya kaskazini (*rogoro*), hii ni kwa sababu lahaja hii haiwezi kutatiza matokeo ya utafiti huu kwa kuwa tofauti kati ya lahaja hizo hueleweka kisemantiki. Mfano *egechuri* hutamkwa kama egesuri, /ch/ hutamkwa kama /s/.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Utohozi si dhana ngeni.Ni jambo ambalo hutokea watu wanaozungumza lugha mbili tofauti wanapowasiliana. Ni dhahiri kuwa jambo hili linapotokea wanaohusika huwa hawana fahamu

kuwa wanatohoa. Waandishi wengi wametoa mawazo yao kuhusu dhana hii. Wengine wameandika vitabu, majarida na hata tasnifu.

### 1.7.1 Dhana ya ukopaji

Ni dhahiri kuwa utohozi husababishwa na ukopaji. Neno lazima likopwe kabla ya kutoholewa. Katika muktadha wa lugha, ukopaji ni kuazima, kuchukua au kukopa maneno kutoka lugha nyingine. Fishman (1968) anasema kuwa ukopaji ni njia ya kuingiza dhana fulani katika lugha nyingine ili kusimamia istilahi ambazo hazipo katika lugha kopaji. Mara nyinyi wakopaji huzingatia tu matamshi wanayoyasikia katika lugha kopeshi na kuweza kuingiza katika lugha kopaji. Hock (1986) anasema lugha huomba maneno kutoka kwa lugha nyingine ili jamii yake iwe na weledi zaidi katika Nyanja za usomi, dini, siasa, sayansi na teknolojia. Apel na Muksen (1987) wanasema kwamba hali ya lugha kuomba maneno kutoka lugha nyingine ni ishara ya lugha kutangamana na lugha nyingine. Poplack (1988) anasisitiza kwamba nomino ndio kategoria ya maneno yanayopatikana katika ukopaji zaidi kwa sababu maneno haya ndiyo yanabeba maudhui katika lugha. Field (2002) anasema nomino zina uwazi wa maana hivyo basi hukopwa kuliko maneno mengine yote. Utafiti huu utaangazia nonimo kama kipashio kuu kinacho toholewa katika lugha ya Ekegusii na kuangazia kanuni kuu zilizo tumika katika utohozi Bynon (1977) anasema kuwa ukopaji ni uhamisho wa maneno ya kileksia kutoka kwa lugha moja hadi nyingine. Naye Mweri (2010) anasema kuwa ukopaji ni hali inayojumuisha uhamishaji wa kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine. Huwa kuna lugha chasili, lugha ambayo neno lililokopwa limetoka na lugha lengwa au lugha inayopokea neno linalokopwa Kwa jumla ukopaji ni kule kujaza pengo la kisemantiki ambalo halina istilahi yake katika lugha asili. Maneno mkopo huwa mara nyingi ni istilahi

zinazopatikana katika taaluma mbali mbali kama vile ya sayansi na teknoloji, asasi za kidini, kijeshi na kadhalika.

Waithaka (2010) ameshughulikia mofolojia ya maneno mkopo ya Gikuyu kutoka Kiswahili, mtazamo wa fonolojia leksia. Tofauti na kazi yetu ni kuwa Waithaka (2010) amejikita mno katika vitenzi. Hata nadharia aliyotumia ni tofauti.

### 1.7.2 Dhana ya utohozi

Utohozi ni utaratibu wa kuyabadili maana au maumbo ya maneno mkopo kutoka lugha changizi ili yalingane na kuafiki mfumo ya sarufi wa lugha pokezi Scotton Myers (2002) anasema kuwa inabidi maneno yanayotoholewa kutoka lugha moja hadi ya pili yafwate utaratibu wa lugha pokezi Ngowa (2015), ametumia nadharia ya fonolojia zalishi katika kuchanganua maneno mkopo ya lugha ya Kigiriama. Utafiti wa Ngowa (2015) ni muhimu kwa utafiti huu wetu kwa jinsi ambavyo umetoa mwangaza wa michakato ya kifonolojia inayopitiwa na maneno ya kigiriama kutoka kwa lugha ya Kiingereza. Tofauti ya utafiti wa Ngowa (2015) na utafiti huu ni lugha zinazochanganuliwa. Utafiti huu unahusisha utohozi wa nomino kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Ekegusii.

Mulwa (2014), ameshughulikia fonolojia ya nomino mkopo za Kikamba. Ametumia nadharia ya fonolojia zalishi. Ingawa ameegemea katika sababu za kiisimu jamii, ameguzia vigezo vya fonolojia na taratibu za utohozi fonolojia. Kazi hii inatofautiana na yetu kwa kuwa lugha pokezi ndizo tofauti. Mwihaki (1998) amechunguza kanuni za fonolojia zinazoongoza utohozi wa maneno mkopo ya Gikuyu kutoka Kiingereza. Vile vile amedhihirisha vigezo vya fonolojia ya Gikuyu. Amesema kwamba lugha ya Kiingereza ina hadhi kubwa ikilinganishwa na Gikuyu kwa sababu imekuwa ikitumika kama lugha rasmi katika maswala ya elimu, sheria na hata serikalini. Nadharia iliyoongoza kazi yake ilitokana na fonolojia zalishi iliyoegemea mtazamo wa fonolojia

tenganishi na fonolojia mizanishi. Kazi hii itakuwa ya umuhimu katika utafiti wetu kwa sababu imeshughulikia utohozi fonolojia katika maneno mkopo ya lugha ya Gikuyu lakini haikugusia utohozi mofolojia wa maneno husika. Isitoshe, utafiti wa Mwihaki (1998) ulilenga utafiti wa lugha zisizo za nasaba moja, utafiti wetu unahusu lugha mbili za Kibantu.

Lugha ya Ekegusii na ya Kiswahili zimeshughulikiwa na watafiti mbalimbali. Utafiti wao umekuwa wa maana katika uchunguzi wetu. Guthre (1948) alitafiti kuhusu lugha za kibantu kwa jumla. Kazi ya Guthre itatuwezesha kutambua ikiwa Kiswahili na Ekegusii ni lugha zenye nasaba moja. Bosire (1993) anaeleza kuwa lugha ya Ekegusii ina lahaja mbili, lahaja ya Kaskazini na lahaja ya Kusini. Tutatumia lahaja ya Kaskazini. Ochichi (2013) ameshughulikia usimbaji maana kimazungumzo katika Ekegusii na Kiswahili. Kazi hii itatufaa kwani katika sura ya tatu anapoangalia kategoria za kisemantiki za Ekegusii, anatilia mkazo nomino na vitenzi vya Ekegusii. Kazi hii itatusaidia kuteua hizo nomino na kutathmini ikiwa zimetoholewa.

Osinde (1988) alishughulikia mabadiliko ya kimofolojia ya konsonanti za Ekegusii. Katika sura ya tatu, alishughulikia kipengele cha nomino na kitenzi. Kazi hii itakuwa ya manufaa kwetu kwani nasi tunashughulikia utohozi wa nomino za Ekegusii.

Obara (2012) ametafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii. Aliangalia makosa ya kifonolojia, makosa ya kimofolojia na makosa ya kisintaksia. Utafiti huu utatusaidia kwa kuwa alieleza kuwa baadhi ya makosa hutokea sababu ya; uchopekaji wa irabu –u, udondoshaji wa sauti –h, uyeyushaji na muundo wa silabi isiyofaa. Utafiti huu utatufaa sana kwani sisi tutachunguza kisababishi cha makosa hayo

Mayaka (2000) alichunguza na kujadili muundo wa sentensi katika lugha ya Ekegusii akitumia nadharia ya sarufi zalishi geuza maumbo. Alitazama sentensi sahili, ambatano na changamano. Kazi hii ni ya maana kwetu ingawa sisi tutatazama silabi sahili, changamano na ambatano.

Mogaka (2009) ameshughulikia fonolojia ya utohozi wa maneno mkopo ya Ekegusii kutoka Kiswahili. Kazi hii inakaribiana sana na kazi yetu. Tofauti ni kwamba Mogaka (2009) hakuangalia ikiwa nomino tohozi zilikuwa na majina asilia naye hakushughulikia mofolojia ya nomino, alijikita katika fonolojia pekee.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Nadharia mbili zimeteuliwa kuongoza utafiti huu, ya kwanza ni nadharia ya ukopaji uhamisho iliyoasisiwa na Odlin (1989) Odlin anaonyesha kwamba utohozi husababishwa na kule kutangamana kwa watu wa kabila tofauti. Nadharia nyingine itakayoongoza utafiti huu ni nadharia ya istilahi ya kisayansi (NIK) nadharia hii imefafanuliwa na Kiingi (1989).

### 1.8.1 Nadharia ya Ukopaji Uhamisho

Nadharia ya ukopaji uhamisho imeasisiwa na Odlin (1989) inasisitiza kuwa wazungumzaji wa lugha mbili wanapotangamana, usambaaji wa vipengele vya lugha kutoka kwa lugha moja hadi nyingine hutokea, huku kutawanyika kwa vipengele vya lugha kutoka kwa jamii moja hadi nyingine huzua dhana za mawasiliano katika mazungumuzo au maandishi.

Nadharia inatazama uwezo wa athari ya lugha ya pili kwa lugha ya kwanza. Odlin (1989) anaona uhamisho huu kama kichocheo kinachosababishwa na mifanano na tofauti ya lugha lengwa na lugha chanzi. Anasema kuwa uhamisho huu kwa kawaida ni kutoka kwa lugha yenye hadhi ya juu kwenda kwa lugha yenye hadhi ya chini.

Odlin alitambua kuwa, kukopa kwa kawaida huanza kwa kiwango cha msamiati. Hii ni kwa sababu chanzo cha athari ya lugha moja kwa nyingine husababishwa na asasi kutoka kwa wazungumuzaji wa lugha nyingine. Kukopa huku kunaweza kuwa na matokeo hasi au matokeo chanya.

Utafiti huu utaangazia nadharia hii ya ukopaji uhamisho ambayo ni kuchunguza uwezo wa athari ya lugha ya pili kwa lugha ya kwanza. Nadharia hii itatuelekeza kuelewa kukopa kutoka kwa lugha ya Kiswahili, yenye hadhi ya juu, hadi lugha ya Ekegusii, lugha ya hadhi ya chini

### 1.8.2 Nadharia ya Istilahi ya Kisayansi (NIK)

NIK ina sifa saba maalum zinazohusu lugha na uendelezaji. Sifa hizo ni pamoja na:

1) Dhana za kimsingi: Inasisitiza kwamba dhana mpya zinapoingia katika jamii tumizi lugha au sehemu ya jamii zinafaa kukopwa lakini sio pamoja na istilahi zake. Dhana inaweza kukopwa lakini iundiwe istilahi 'faafu'
2) Kila kinachojenga nadharia halisi ni madai yanayokubalika (kuhusu kipindi cha majaribio ya istilahi katika medali ya sayansi)
3) Sheria ya uundaji wa istilahi huongoza katika kutambua usawa wa sentensi kisayansi na kuwepo au kutokuwepo kwa istilahi fulani katika lugha za kurejelea dhana mpya.
4) Mfumo wa kivipindi wa arki za kidhana: hii ni sifa mojawapo ya NIK inayojumlisha elementi au arki za kidhana zinazopatikana katika ubongo wa binadamu.
5) Sheria ya uundaji istilahi ya ugeuza maumbo kidhana (UMK) sheria ya UMK inasisitiza kwamba istilahi mpya hujenga au huzalishwa pasi na kuzingatia lugha tunayoitumia katika mazungumzo.
6) Sifa inayohusu sheria ya kuziba mapengo. Kutokana na sifa hii muhimu ya NIK, swala linalosisitizwa ni vitambulishi vya dhana. Waundaji istilahi za Kiswahili wanapaswa kufahamu vitambulishi vya dhana zilizomo katika Kiswahili na kuundia dhana hizo istilahi mwafaka.
7) Sifa nyingine inahusu vigezo vya istilahi 'faafu' vya PEGITOSCA. Misingi na vigezo vya istilahi 'faafu' italeta usasa na usawa au upatanisho wa kimataifa katika shughuli za ukuzaji wa istilahi za lugha mbalimbali duniani (zingatia vigezo vya PEGITOSCA)

Maana ya 'usayansi katika mbinu' ni uwezo wa mbinu za uundaji istilahi za lugha kufanyiwa uchunguzi, ili kutambua 'ufaafu' wa kila mojawapo, kwa kuzingatia misingi na kanuni za lugha

husika, katika utafiti huu tutatazama kanuni za lugha ya Ekegusii. Nadharia hii iliasisiwa na K.B. Kiingi (1989) Kiingi anajadili kwa mapana vigezo tisa vya "ufaafu" wa istilahi. Vigezo hivyo vinajenga akronimu PEGITOSCA

| | | |
|---|---|---|
| P | precision | udhahiri |
| E | economy | iktisadi |
| G | generativity | uzalishaji |
| I | internationality | umataifa |
| T | transparency | uangavu |
| O | non- obscenity | utusani |
| S | systemicity | utaratibu maalum |
| C | consistence | utaratibu ulio sawa |
| A | appropriateness | ukubalifu/ufaafu |

Kigezo muhimu zaidi cha ufaafu wa istilahi ni udhahiri. Istilahi lazima iwe isiyotatanisha mtumiaji wake. Istilahi bora ni ile inayolenga maana ya dhana inayotumiwa kwa udhahiri bila utata.Kwa mfano,

'Salt'----------- chumvi

Neno chumvi linaweza kuwa na utata kwa sababu chumvi ni za aina nyingi, kuna kloridi, nitrati, fostati, zulfati n.k. tunaamini kwamba neno munyu ingawa linatokana na msamiati asilia wa Kiswahili, ni dhahiri zaidi na linakubalika na watumiaji wa Kiswahili.

Kigezo cha iktisadi kinamaanisha ufupishaji wa istilahi kikundi kwa kuviunga vipashio tenzi vya istilahi hiyo ili kupata istilahi fupi. Kila lugha hulenga ufupi wa matamshi na maneno. Istilahi ndefu mno haisaidii katika sifa hii. Kwa mfano:

"mwanawingilugha"--------mlumbi

Kigezo cha uzalishaji kina maana kuwa Istilahi faafu iweze kuzalisha maneno zaidi kwa mnyambuliko. Katika Kiswahili, mofimu '—isha' ni zalishi, inanyambulika na inaweza kutumika kuunda istilahi nyingi. Kigezo cha umataifa kinafafanua kuwa si lazima istilahi za isimu ya Kiswahili ziswahilishwe kutoka istilahi za kiingereza zilizotokana na kigiritini lakini zichukuliwe kama ishara zilizokubalika kimataifa

Katika kigezo cha uangavu, kinacho chunguzwa hapa ni uhusiano wa istilahi za isimu ya Kiswahili na maana. Istilahi iangaze maana. Uangavu wa istilahi hutegemea mtumiaji wake. Maana ya kigezo cha utusani ni kwamba istilahi iepuke maana ya matusi kulingana na adabu ya lugha ya jamii lengwa. Istilahi zenye stara zinafaa kuundwa. Istilahi "chafu" kiutamaduni haziwezi kukubalika kama istilahi "faafu" za lugha husika.

Mfano------"penis" mboo (kizalishi/ume—kinachomshikisha mke mimba)

"emboro" Ekegusii.

Kigezo cha utaratibu maalum ambacho utafiti huu utatumia kwa mapana kina maana kuwa istilahi iundwe kuambatana na utaratibu fulani wa kuunda. Istilahi zisiundwe kiholela na bila kufuata utaratibu dhahiri. Hiki kigezo kitatumika sambamba na kigezo cha utaratibu ulio sawa. Kigezo hiki kinasisitiza istilahi kuwa nyofu na kuundwa kuambatana na utaratibu thabiti. Kigezo cha ukubalifu na ufaafu wa istilahi ndiyo azma ya mwana leksikografia. Ukubalifu na ufaafu wa istilahi huambatana na hadhi ya kitaifa au jamii tumizi lugha yenyewe. Kuhusu mpangilio wa vigezo na kanuni za istilahi kutokana na 'ubora' wa kila mojawapo, Kiingi (1989) anatoa hatua tatu kuwa:

a) Udhahiri na utaratibu maalum ni vigezo muhimu zaidi na vinachukua nafasi ya kwanza.

b) Iktisadi na uzalishaji ni vigezo muhimu vinavyochukua nafasi ya pili.

c) Vigezo vyote vilivyosalia vinachukua nafasi ya tatu na ya mwisho: umataifa, uangavu,utusani na ukubalifu/ufaafu.

Uzingatiaji wa usayansi na kaida za istilahi za isimu ya Ekegusii utasaidia katika kuchagua istilahi faafu zaidi kunapotokea ushindani miongoni mwa visawe vinavyotumika kuwakilisha dhana moja. Tatizo la utata na wingi wa visawe litapunguzwa kama ilivyo katika:

Uwiano wa irabu

Ulinganifu wa irabu

Upatanishowa irabu

Utangamano wa irabu

Mifanyiko ya kifonolojia

Michakato ya kifonolojia

Taratibu za kifonolojia

## 1.9 Mbinu Za Utafiti

Nomino tohozi kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Ekegusii zilizochunguzwa zilidondolewa kutoka kwa radio. Mtafiti ambaye ana tajriba katika lugha inayotafitiwa alisikiliza vipindi teule, stesheni ni ya *Egesa F.M.* Stesheni hii hufululiza vipindi vyake kwa Ekegusii, kipindi teule ni 'Taarifa ya habari' inayoletwa hewani kila siku saa tatu ya jioni. Data ilikusanywa kwa jumla ya wiki mbili.

Data nyingine ilikusanywa katika kanisa la SDA ya Gesieka, kanisa hii ilichaguliwa kwa sababu mahubiri hutekelezwa kwa lugha ya Ekegusii. Kwa kuwa kulikuwa na maombi kanisani juma nzima Aprili tarehe 11 hadi 16, mtafiti alijiunga na wakristo wengine huku akinukuu maneno tohozi. Pamoja na kusikiliza mahubiri katika lugha ya Ekegusii, Taasisi ya ukuzaji mitalaa nchini Kenya (KICD) (2004) itatumika. Uchunguzu wa kimaktaba utatumika katika utafiti huu,

tulidurusu na kusoma tasnifu za Kiswahili, tasnifu za Kiingereza, vitabu, magazeti na majarida. mbalimbali yaliyokuwa na makala yanayohusiana na mada hii.

### 1.1 0 Kukusanya Data

Data iliyokusanywa ni ya nomino. Data hii ilikusanywa kutoka matini andishi ya Ekegusii. Matini iliyorejelewa ni Biblia ya Ekegusii, K.I.C.D. (2004) tusome lugha yetu (Ekegusii) K.I.C.D. (1987). Data nyingine ilikusanywa kutoka kwa redio. Mtafiti alisikiza matangazo kwa lugha ya Ekegusii stesheni ya *Egesa*, data ya radio ilikusanywa kwa muda wa majuma matatu. Haya yaliwezekana kwa sababu mtafiti ana tajriba kubwa katika lugha pokezi. Kamusi ya Ekegusii (Endabasi) ilitumika katika kuhakikisha uhalisia wa maneno tohozi. Nomino tohozi zilizokusanywa ziliwasilishwa kwa wazungumuzaji asilia wa lugha hii walioombwa kusoma nomino hizo kwa njia ya uasilia. Kinasa- sauti kilitumika katika utafiti huu tulipowahoji hao wazungumuzaji katika harakati ya kutaka kujua majina asilia ya nomino hizo na matamshi bora ya nomino tohozi, Kinasa-sauti kilisaidia hasa wakati ambapo mtafiti alikosa kusikia matamshi ya nomino nyingine, aliweza kusikiliza kanda hizo baadaye na kupata matamshi halisi. Mahojiano haya yalidumishwa kwa mahusiano mazuri ili ukusanyaji wa data usikatizwe kwa njia yoyote Mugenda (1999).

### 1.11 Kuchanganua Data

Data iliyokusanywa kwenye utafiti huu ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Baada ya kutoka nyanjani, tulikusanya maneno yote yaliyotafitiwa, tukateua yaliyotoholewa. Nadharia ya ukopaji uhamisho iliyoasisiwa na Odlin (1989) ilitupa mwelekeo. Nadharia hii inaelekeza kuwa maneno tohozi ni yale yaliyosababishwa na usambaaji wa vipengele vya lugha kutoka kwa lugha moja hadi nyingine. Hivyo tulitenga nomino zilizo na vipengele vya lugha chanzi kisha tukachunguza tofauti na ufanano uliopo.

Baadhi ya haya maneno ni yale tuliyoyadondoa kutoka kwa Kamusi ya Ekegusii (Endabasi) Tuliainisha sauti ili kubainisha zilizogeuka. Mageuko haya ya sauti yalielezwa kutegemea kanuni za fonolojia ya Ekegusii. Katika uchanganuzi huu, tulizingatia nadharia ya istilahi ya kisayansi iliyoasisiwa na Kiingi, (1989). Tukirejelea nadharia ya NIK tulitambua kuwa istilahi za Ekegusii zimefuata utaratibu fulani, aidha kimofolojia au kifonolojia. Jumla ya nomino 78 ziliteuliwa kutoka kwenye orodha ya nomino tohozi zilizokusanywa. Idadi hii ya nomino ilichukuliwa kuwa toshelevu. Vigezo viwili vilitumiwa katika kufanyia majaribio nomino hizi.

Kigezo cha umbo la istilahi (kimofolojia)

Kigezo cha aina ya mfanyiko uliotumika kuunda istilahi (kifonolojia)

Tuliegemea katika kigezo cha udhahiri (istilahi lazima iwe isiyotatanisha mtumiaji wake) na kigezo cha utaratibu maalum (istilahi iundwe kuambatana na utaratibu fulani wa kuunda). Sifa mojawapo ya tathmini ya kisayansi ni kueleza kwa ukamilifu kile kinachoonekana, na hivyo katika kigezo cha pili 'kigezo cha aina ya mfanyiko uliotumika katika kuunda istilahi' ulitufungua macho kuona usayansi uliopo na " ufaafu" wa nomino hizo.

# SURA YA PILI

# UASILIA WA MSAMIATI

## 2.1 Utangulizi

Nomino za Ekegisii huwa na sehemu mbili kimuundo, mwanzo na shina. Kuna njia kadha za uundaji wa nomino. Mofolojia ya uundaji maneno ni mchakato unaotegemea uambishaji. Katika utafiti huu Tutataka kujua iwapo nomino zote zizilizotoholewa kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Ekegusii zilikuwa na majina asilia katika lugha ya Ekegusii na nomino hizo zilichukua muundo upi wa utohozi. Nomino zitakazozingatiwa katika utafiti huu ni nomino-zilizo na asili ya Uarabuni na maneno ya Kiswahili sanifu.

## 2.2 Sayansi na teknolojia

Kutokana na uvumbuzi wa kisayansi, binadamu wamezua maneno ambayo hutumika katika Nyanja za kisayansi na teknolojia ambayo hayapatikani katika Ekegusii. Jambo hili limesababisha istilahi hizo kutoholewa moja kwa moja ili kuafiki mawasiliano na utangamano baina ya watumiaji wa Ekegusii. Jedwali nambari 2.1 linaangazia baadhi ya istilahi hizo.

**Jedwali: 2:1 Sayansi na teknolojia**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino Asilia |
|---|---|---|
| Ratiri | Eratiri | - |
| Randa | Eranda | - |
| Simu | Esimi | - |
| Sindano | Esindani | - |
| Saa | Ensa | - |

| | | |
|---|---|---|
| Makasi | Amagasi | - |
| Ufunguo | Ekebunguo | - |
| Pesa | Ebesa | - |
| Gari | Egari | - |

Nyanja hii ya sayansi na teknolojia haina hata neno moja lililokuwa na jina asilia, hii ni kwa sababu ya uchangamano uliopo katika nyanja hiyo Kwa kuwa huu ni uwanja wa kiufundi Abagusii hawakuwa na vifaa vilotajwa hapo juu, kwa kuwa ilibidi mawasiliano yaendelezwe ilibidi Abagusii wayatohoae maneno hayo ili pawepo na mawasiliano.

### 2.3 Isitlahi za kimasomo

Kutokana na maajilio ya wamishonari, elimu ya kisasa iliweza kujipenyesha katika eneo la Abagusii. Kutokana na elimu hiyo, istilahi za kimasoma ziliibuka ambazo hazikuwa na majina asilia ya Ekegusii na hivyo ikabidi utohozi ufanywe kwa Kiswahili na hatimaye kwa Ekegusii kama inavyoangaziwa katika jedwali 2.2

**Jedwali 2.2 Isitlahi za kimasomo**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino asilia |
|---|---|---|
| Mwanafunzi | Omwanafunsi | - |
| Kalamu | Ekaramu | - |
| Kitabu | Egetabu | - |
| Sanduku | Esanduki | - |

| | | |
|---|---|---|
| Mfuko<br>Meza<br>Mlango<br>Karatasi | Omoguko<br>Emesa<br>Omorangu<br>Ekaratasi | -<br>-<br>Ekige<br>- |

Katika utamaduni wa Abagusii, msamiati wa elimu rasmi haukuwepo, hii ni kwa sababu walikuwa na njia yao ya kipekee walivyopokea elimu. Elimu waliyopokeza kila kizazi ni ya imani na itikadi za jamii yao na haikuhusisha kwenda shuleni wala kuandika. Kutokana na utamaduni mpya wa kielimu lugha ya Ekegusii ilikopa msamiati unaohusu taaluma hiyo, wakalazimika kutohoa maneno moja kwa moja.

**2.4 Msamiati wa jikoni**

Hata kabla wageni waje nchini Kenya, jamii ya Omogusii ilikuwa na njia zake tofauti za kujimudu, vyakula vilikuwepo pamoja na vyombo vya kuandaa hicho chakula na hata vya kupakulia na kulia. Tofauti ni kuwa vyombo walivyoleta hawa wageni vilikuwa tofauti na havikuwa na majina asilia hivyo ikabidi majina yao yatoholewe kutoka Kiswahili. Licha ya hayo, kuna vifaa vilivyoletwa na wageni na vikawa vinatekeleza kazi ya vifaa asilia hata kama kimuundo vilionekana tofauti na vile asilia kama jedwali 2.3 linavyoonyesha. Tofauti ya kimuundo ndiyo iliyosababisha majina asilia kufifia na majina tohozi kuchukua nafasi yao.

**Jedwali 2.3 Msamiati wa jikoni**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino Asilia |
|---|---|---|
| Kikombe | Egekombe | Egetabo |
| Kijiko | Egechiko | Omogango/ekeburugo |
| Kiberiti | Ekebiriti | Ogosegesa |
| Sahani | Esani | Ekee |
| Chungu | Enyongo | Egetono |
| Bakuli | Ebakuri | Egetabo |
| Kibuyu | Ekebuyu | - |
| Jiko | Echiko | - |

Mlo ulikuwepo tangu jadi, ndio maana msamiati huu wa jikoni ulikuwa na maneno asilia, hata hivyo ni kana kwamba maneno haya yamepitwa na wakati. Watumiaji lugha hii ni wachache sana wanaoujua msamiati huo asilia, hasa kisasi kipya.

## 2.5 Msamiati wa mavazi na mapambo

Omogusii hakuwa na mavazi mengi ila kulikuwa na tofauti kati ya mavazi ya kiume na kike. wanaume walivaa "*Egesena*" huku wanawake wakivaa '*Engobo*". Egesena ni aina ya vazi lililotumika kuficha sehemu za siri za mwanaume. Haikujalisha iwapo sehemu ya juu ilifunikwa. Hivi sasa kuna mavazi aina nyingi na ambayo majina yao yametoholewa kutoka Kiswahili hadi Ekegusii kama inavyodhihirika katika jedwali 2.4

**Jedwali 2.4 Msamiati wa mavazi na mapambo**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino Asilia |
|---|---|---|
| Suruari | Esiruari | Egesena |
| Kofia | Egobi | Egutwa/egutu |
| Sidiria | Egesindereo | - |
| Buibui | Ebuibui | - |
| Kirinda | Amarinda | - |
| Kabuti | Ekabuti | - |
| Kitenge | Egetenge | - |
| Kanzu | Ekanzu | - |
| pete | Ebete | - |
| kitambaa | Egetambaa | - |
| Leso | Ereso | - |
| Kiatu | Egeato | - |

Hapo awali hapakuwa na mavazi mengi, Vazi lolote hapo awali lilikuwa na jina moja la jumla *engobo,* tofauti na wakati huu ni kuwa kila vazi linatambuliwa na sehemu linalovaliwa na kupewa jina maalum. Mavazi kama vile kanzu na buibui ni mavazi yaliyovaliwa na waswahili hivyo hayakuwapo.

## 2.6 Msamiati wa dini

Hapo awali Abagusii walikuwa na dini na njia zao za kuabudu Mungu wao aliyeitwa "Engoro". Tofauti ni kuwa hawakuhusisha mambo mengi kwenye harakati zao kama ilivyo sasa. Kutokana na maajilio ya wamishonari walioleta dini ya kisasa, kulitokea msamiati wa kidini ambao ulitoholewa ili kuafiki matakwa ya kidini katika jamii hii husika kama inavyoelezwa katika jedwali 2.5

**Jedwali 2.5 Msamiati wa dini**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino asilia |
|---|---|---|
| Sadaka | Esataka | - |
| Kanisa | Ekanisa | - |
| Kurani | Ekorani | - |
| Yesu | Yeso | - |
| Sala | Esara | - |
| Madhabau | Amadhabau | - |
| Kengele | Ekengere | - |

Dini ililetwa Afrika masharki na wamishonari na wakoloni ambao ilibidi wafunze waafrika lugha ya Kiswahili kusudi waweze kuwasiliana. Katika harakati hiyo, maneno ya kidini yalitoholewa ingawa mengi yao yalifuata mkondo wa utohozi tafsiri (utohozi tafsiri ni utohozi ambao neno) linatafsiriwa jinsi maana yake ilivyoeleweka mfano:

**Jedwali 2.5.1 Utohozi Tafsiri**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Tafsiri |
|---|---|---|
| Kanisa | Ekanisa | Nyumba ya Muumba |
| Yesu | Yeso | Omotongi |
| Sadaka | Esataka | Ebiegwa |

## 2.7 Msamiati wa wanyama

Majilio ya wageni hayakuchangia katika kuleta wanyama. Wanyama wa pori walikuwepo na walikuwa na majina yao asilia licha ya kuwa majina haya yamefifia sana kutokana na utohozi wao kutoka kwa Kiswahili hadi Ekegusii. Jedwali 2.6 linatuelezea matokeo haya.

**Jedwali 2.6 Msamiati wa wanyama**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino asilia |
|---|---|---|
| Punda | Ebunda | Etigere |
| Ng'ombe | Eng'ombe | Esabagera |
| Farasi | Ebarasi | - |
| Simba | Esimba | Endo |
| Chui | Echui | Ekwachi/engo |
| Mbuni | Embuni | Esagero |
| Twiga | Etwega | Esirori |
| Ngamia | Engamia | - |
| Nyuni | Enyoni | - |

Licha ya kufifia kwa majina hayo, bado baadhi yao yanaendelea kutumika. Totauti kati ya nomino hizo katika Ekegusii na Kiswahili ni kuwa katika Ekegusii zimetangulizwa na vokali /e/ ili kuafiki muundo wa lugha tohozi. Tofauti ni katika neno punda ambapo /p/ imegeuka na kuwa /b/ nayo /f/ ikageuka ikawa /b/ katika neno farasi (maelezo zaidi yametolewa katika sura ya nne, data inapochanganuliwa)

## 2.8 Msamiati wa vyakula

Awali Abagusii walikuwa na vyakula vyao asili ambavyo vingali vipo na kwa kuwa wageni hawakuvitambua, hawakuwa na majina yao hivyo nyingi ya nomino hizo hazijatoholewa.

**Jedwali 2.7 Msamiati wa vyakula**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino asilia |
|---|---|---|
| Munyu | Omonyo | Ebara |
| Chumvi | Echumbi | - |
| Kitunguu | Egetunguo | _ |
| Viazi | Ebiasi | - |
| Mchele | Omochere | - |

Vingi vya hivi vyakula havikuwepo ndio maana havina majina asilia.

## 2.9 Siku za wiki

Majina ya wiki yalikuwepo tangu jadi, Abagusii walikuwa na majina waliotumia kurejelea kila siku, hata hivyo, ni wachache mno wanaodai kuwa wenyeji wa lugha hii wanajua hayo majina asilia,wengi wanatumia majina tohozi kama vile jedwali 2.9 linavyoonyesha.

**Jedwali 2.8 Siku za wiki**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Nomino asilia |
|---|---|---|
| Jumapili | Chumapiri | Omokubio |
| Jumatatu | Chumatato | Etichi rimo |
| Jumanne | Chumaine | Etichi kabere |
| Jumatano | Chumatano | Etichi gatato |
| Alhamisi | Aramisi | Etichi kane |
| Ijumaa | Ichuma | Eriatano |
| Jumamosi | Chumamosi | Enyongesa |

Abagusii walitambua siku za wiki na siku hizo zote zilikua na majina asilia. Katika utohozi walibadili /y / ikawa /ch/ na mengine yakabaki vile. Mageuko haya yameelezwa zaidi katika sura ya nne.

## 2.10 Majira na nyakati

Majira na nyakati vilikuwepo tangu jadi, Abagusii hawakuwa na majina maalum waliyoyatumia kuvirejelea. Hata hivyo, ishara na matukio tofauti ya hali ya anga yaliwaelekeza kutambua majira yaliyojiri. Mfano, upepo mwingi, jua kali na majilio ya wanyama tofauti haswa ndege ilikuwa ni ishara ya kiangazi

**Jedwali 2.9 Majira na nyakati**

| Kiswahili | Nomino tohozi katika Ekegusii | Asilia |
|---|---|---|
| Kiangazi | Ekiangazi | Omorakera |
| Leo | Rero | _ |
| Magharibi | Mogoroba | _ |
| Juma | Echuma | _ |
| Mwaka | omwaka | _ |

## 2.11 Sehemu za Mwili

Bali na kuwa haya ni maumbile ya Mungu, hakuna sehemu ngeni iliyoletwa na wageni, sehemu zote za mwili zina majina yao asilia na sehemu zote hazikutoholewa kama linavyoonyesha jedwali 2.10

**Jedwali 2.10 Sehemu za mwili**

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Kichwa | Omotu |
| Nywele | Etuki |
| Sikio | Ogoto |
| Shavu | Emboto |
| Ulimi | Oromeme |
| Titi | Orobere |

Nomino zingine zilitoholewa lakini kama vile jedwali 2.10.1 linaonyesha.

**Jedwali 2.10.1 Sehemu za mwili zilizotoholewa**

| Kiswahili | Ekegusii | Asilia |
|---|---|---|
| Jino | Erino | Ebitakunero |
| Jicho | Eriso | Endorero |
| Mgongo | Omogongo | - |
| Moyo | Omoyo | Enkoro |
| Mguu | Okogoro | - |

## 2.12 Hisabati

Hata kama Abagusii hawakuwa na masomo rasmi, jinsi ilivyo wakati huu, walikuwa na njia yao ya kuhesabu na hali ya kutathmini hisabati bila ishara tulizo nazo sasa. Mfano, walihesabu mifugo, mashamba na mali yao.

**Jedwali 2.11 Hisabati**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Asilia |
|---|---|---|
| Ishirini | Isirini | Emerongo ebere |
| Thelathini | Sarasini | Emerongo etato |
| Arubaini | Arobaini | Emerongo ene |
| Hamsini | Amisini | Emerongo etanoemo |
| Sitini | Oisitini | Emerongo etanoemo |
| Sabini | Sabiini | Emerongo etanoebere |

| | | |
|---|---|---|
| Themanini | Tamanini | Emerongo etano etato |
| Tisini | Tisaini | Emerongo kianda |
| Mia | Emi | Rigana erimo |
| Elfu | Eeribu | - |
| Milioni | Emirioni | - |

## 2.13 Nominoambata

Nominoambatano ni nomino ambazo zimeundwa kwa maneno mawili au zaidi kuchukuliwa na kuunganishwa kuunda nomino moja. Kama vile msamiati wa dini ulifuata mkondo wa utohozi tafsiri, nazo nominoambata zilifasiriwa vivyo hivyo. Kwa kuwa hizi zimeundwa na nomino mbili, utohozi pia ulifuata mkondo huo bali waliongeza vokali mwanzoni mwa nomino ili kuafiki mtindo wa lugha ya Ekegusii.

**Jedwali 2.12 Nomino ambatano**

| Kiswahili | Nomino Tohozi katika Ekegusii | Asilia |
|---|---|---|
| Mwananchi | Omwanainchi | - |
| Mfanyabiashara | Omonyabiasara | Omoonchoreri |
| Mwanakijiji | Omwanakijiji | Omonyakenyoro |
| Mwanasiasa | Omwanasiasa | - |

## 2.15 Hitimisho

Katika sura hii tumetazama iwapo nomino za Ekegusii zilikuwa na majina asilia. Tumegawa nomino hizi katika makundi mbali mbali. Tumetazama msamiati wa sayansi na teknolojia, jikoni, mavazi, dini, wanyama, vyakula na vinywaji, majira na nyakati, siku za wiki na sehemu za mwili. Utafiti huu umedhihirisha kuwa nomino nyinyi zilizo katika lugha ya Ekegusii zimetoholewa kutoka kwa maneno ya asili ya Kiswahili sanifu na maneno ya asili ya Kiarabu. Hata hivyo imedhihirika pia kuwa ingawa baadhi ya nomino zina majina asilia tena nomino hizo zimetoholewa. Utohozi huu umesababisha majina ya nomino asilia kuwa mfu. Hii ni kusema kuwa maneno tohozi ndio hutumika sana.

Nyanja ya siku za wiki umekopa asili mia moja lakini tena ulikuwa na nomino asilia asili mia moja, hii ni kwa sababu walikuwa na njia zao za kipekee za kutambua siku na nyakati. Nyanja ya msamiati wa jikoni pia umekopa asili mia moja, tofauti ni kuwa neno moja asilia lilirejelea vitu zaidi ya moja. Mfano kikombe, sufuria na sahani vyote viliitwa *egetabo*. Msamiati wa mavazi nao ulifuata mkondo huu, koti, sweta, na longi vyote vilijulikana kama engobo. Msamiati wa dini pia ulitoholewa mno na tena ulionekana kuwa na majina asilia ila majina haya asilia tena yalikuwa ya utohozi tafsiri. Ni dhahiri kuwa nyanja ya masomo, nomino vifaa, vyakula na vinywaji havikuwa na majina asilia mengi hii ni kwa sababu aina ya masomo yalokuwapo hapo awali yanatofautiana mno na masomo ya kisasa yanayojumuisha kusoma na kuandika. Vyakula navyo vinavyoliwa wakati huu ni tofauti na vyakula vya hapo jadi. Utafiti huu umedhihirisha kuwa nyanja ya sayansi na teknolojia imetohoa msamiati wote. Hii ni kwa sababu hii ni nyanja ya kiufundi wa kisasa.

# SURA YA TATU

# MOFOFONOLOJIA YA EKEGUSII

## 3.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu mofofonolojia ya maneno tohozi unavyotegemea vigezo vinavyodhihirika katika mfumo wa lugha ya Ekegusii. Kuna haja ya kushughulikia vigezo hivyo kwani ndivyo vitaweka wazi utaratibu unaotumika katika utohozi. Nadharia iliyotumika kuchunguza vigezo hivyo ni ile ya NIK. Nadharia hii inatumia usayansi kuweka wazi vigezo vya kimofofonolojia ya Ekegusii, vigezo vilivyoshughulikiwa ni pamoja na viambishi awali, ambavyo vimeshughulikiwa katika sura ya pili, silabi na fonimu. Kigezo cha saba cha NIK ambacho ni utaratibu maalum kinasisitiza istilahi iundwe kuambatana na utaratibu fulani wa kuunda istilahi kiholelaholela na bila kufuata utaratibu dhahiri.

Katika sehemu hii maelezo mafupi kuhusu fonimu za Ekegusii na za Kiswahili yatatolewa, nia ya kutoa maelezo haya ni pamoja na kutoa mwongozo wa jinsi mageuzi ya kimofofolojia yanavyotokea. Hii ni kwa sababu utafiti huu umeegemea katika michakato ya kimofofonolojia inayopitiwa na fonimu wakati wa utohozi.

Fonimu ni kipashio muhimu sana katika taaluma ya fonolojia. Ni kiungo cha kimsingi katika uhakiki wa sauti katika lugha mahususi Obuchi na Mukhwana (2010). Ni kitengo cha sauti yoyote ya lugha inayobainishwa kimatamshi katika maneno ya lugha lengwa. Lugha ya Ekegusii ina fonimu za aina mbili ambazo ni vokali na konsonanti.

Fonolojia ni taaluma inayoshughulikia mpangilio wa sauti katika lugha yaani namna sauti zinavyojumlishwa kwa pamoja na kupangiliwa ili kuunda maneno. Kila lugha ina namna yake ya kupanga sauti zake ili kutofautisha na lugha nyingine zote ulimwenguni. Mathalan Kiswahili

hutumia umbo la kvkv (konsonanti ikifwatwa na vokali) Gibbe (1987). Lugha ya Ekegusii ambayo tayari tumesema ni ya nasaba moja na Kiswahili vile vile hufuata mkondo ule ule wa kvkv kuunda maneno yake.

## 3.2 Vokali za Ekegusii

Vokali ni fonimu ambazo hutumia nguvu hafifu katika utumiaji wake, Mgullu (1999). Wana fonolojia wanatambua kwamba vokali ni sauti hafifu kwa sababu ya ule urahisi wake wa jinsi ya kutamka. Ni vyema kuelewa mfumo wa vokali za Ekegusii katika utafiti huu kwa sababu ni baadhi ya fonimu zinazopitia mageuzi tofauti tofauti ya kimofolojia katika utohozi

Hapo awali iliaminika kwamba lugha nyingi za kibantu huwa na irabu kati ya tano na saba, hata hivyo kuna baadhi ya tafiti ambazo zinaonyesha kuwa lugha nyingi za kibantu zina irabu ya zaidi ya kumi. Otiende (2013) katika kutazama Athari za Kimofofonolojia za Kiolosuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili amekubaliana na maoni ya Ogechi (2012) anapozilinganisha Ekegusii na IgiKuria na kueleza kwamba lugha hizo mbili hudhihirisha irabu saba zikiwemo irabu tano ndefu na tano fupi. Utafiti wetu unaelekeza kuwa irabu za Ekegusii ni saba Irabu hizi ni : /a/ /e/ /ɛ / /i/ /o/ /ɔ/ /u/ pamoja na hizi kuna irabu tano za wakaa mrefu ambazo ni /a:/ /e:/ /i:/ /o:/ / u:/

**Jedwali 3.1Vokali za Ekegusii**

Tayari tumesema kuwa vokali ni fonimu ambazo hutamkika kwa njia rahisi. Kwa maelezo zaidi angalia 3.2.

| Sauti | Maneno | Maana |
|---|---|---|
| a | [amate] | Mate |
| a: | [ega:ri] | Gari |
| e | [egoti] | Koti |
| e: | [ebende:re] | Bendera |
| ɛ | [esese] | Kikohozi |
| i | [ira] | Chukua |
| i: | [eči:ko] | Jiko |
| o | [igoro] | Juu |
| o: | [oburo:ti] | Ploti |
| ɔ | [igɔrɔ] | Jana |
| u<br>u: | [etuba]<br>[ebu:ndi] | Tupa<br>fundi |

Vokali zinaweza kuwa vianzio vya nomino, katikati ya nomino lakini lazima vokali iwe mwisho wa nomino. Utaratibu unaoongoza jinsi ya kutamka hizi vokali ni utandazo wa ulimi, mkao wa midomo na mwiniko wa ulimi.

### 3.3 Sehemu ya Kutamkia Vokali ya Ekegusii

**Jedwali 3.2 Vokali ya Ekegusii**

| Uinuko wa ulimi | Ulalo wa ulimi | | |
|---|---|---|---|
| | Mbele | Katikati | Nyuma |
| .Juu | i | | u |
| Kati juu | e | | o |
| Kati chini | ɛ | | ɔ |
| Chini | | a | |

### 3.4 Konsonanti za Ekegusii

Konsonanti ni fonimu ambazo wakati wa kuzitamka mkondo hewa wa matamshi huzuiliwa kwa namna fulani na kwa kadiri tofauti Ladefoged (2005) na Hyman (1975). Utafiti huu unaonyesha kuwa lugha ya Ekegusii hujumuisha mfumo wa konsonanti 21 tofauti na Mogaka (2009) aliyetambua konsonanti 21. Mogaka (2009) alirudia fonimu/r/ /m/ na /y/ na kuacha fonimu /u/ na /w.

**Jedwali 3.3 Konsonanti za Ekegusii**

| Fonimu | Othografia | Neno | Maana |
|---|---|---|---|
| [ß] | b | [aßarimu] | walimu |
| [mb] | mb | [embuni] | mbuni |
| [č] | ch | [ečuma] | chuma |
| [nd] | nd | [endege] | ndege |
| [g] | g | [egarani] | galani |
| [ŋg] | ng | [eŋgumi] | ngumi |
| [ŋ] | ng' | [eng'ombe] | ng'ombe |
| [k] | k | [ekabati] | kabati |
| [m] | m | [omonto] | mtu |
| [n] | n | [enauri] | nauli |
| [nk] | nk | [nka] | nyumbani |
| [nch] | nch | [nchwo] | njoo |
| [ns] | ns | [nse] | chini |
| [nt] | nt | [ntebi] | niambie |
| [ny] | ny | [enyama] | nyama |
| [r] | r | [erekoti] | rekodi |
| [s] | s | [esini] | sinia |
| [t] | t | [etochi] | tochi |
| [u] | u | [ukoma] | ukoma |
| [w] | w | [bwari] | jina la mtu |
| [j] | y | [yaerire] | imeishia |

Kwa mujibu wa Mwalo (2002) Mohammed (2001) anaeleza kwamba kwa kawaida, konsonanti hutumika katika mazingira ya awali kama konsonanti sahili au kama konsonanti changamano. Katika Ekegusii, nomino nyingi huanza na vokali wala sio konsonanti ni katika wingi wa nomino zinapoanza na vokali, mfano

**Jedwali 3.4 Wingi wa nomino**

| Umoja/kis | Wingi/kisw | Umoja/Ekeg | Wingi/Ekeg |
|---|---|---|---|
| [Sahani] | Sahani | [Esani] | Chisani |
| [Diriša] | Madirisha | [Etirisa] | Chitirisa |

Kama ilivyo katika uchanganuzi wa kifonolojia kwa jumla, konsonanti za Ekegusii zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia jinsi ya kutamka na pahali pa kutamkia. Kulingana na sifa za mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka. Kwa kuzingatia mahali pa kutamkia tunapata konsonanti za aina mbili, vikwamizo na vifulizo. Vikwamizo ni vya aina nne: Vipasuo, vizuiwa, vikwamizwa na nazalishi. Vifulizo hutambua aina tatu za konsonanti: nasali, vilainisho, na nusu irabu Jedwali lifuatalo linawakilisha muhtasari huu.

**Jedwali 3.5 Sehemu za kutamukia konsonanti za Ekegusii**

| Jinsi ya kutamka | Pahali pa kutamkia | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Midomoni | Ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini |
| Vikwamizo | Vipasuo | | t | | K |
| | Vizuiwa | | | č | |
| | Vikwaruzo | ß | s | | |
| | Nazalishi awali | Mb | nt,nd,ns | ɲč | ɲk ɲg |
| Vifulizo | Nazali | m | n | ɲ | ɲ |
| | Vilainisho | | r | | |
| | Viyeyusho | w | | J | |

**Jedwali 3.6 Matumizi ya Fonimu /j/**


| Neno | Kiswahili | Wakati |
|---|---|---|
| a) Nayire | Nimechomeka | Uliopo |
| b) Inayiete | Nimechomwa | Uliopita |
| c) Ninyie | Nitachomeka | Ujao |
| d) Ninyjiete | Nilichomeka | Uliopita kitambo kidogo |

Katika (d), ni lazima /j/ iongezwe ili maana ieleweke vyema kuwa ni kuhusu kuchomeka la sivyo /j/ ikiondolewa maana ya neno itabadilika iwe kulowa majini.

## 3.5 Vokali za Kiswahili

Wakati wa kushugulikia irabu mwanaisimu Daniel Jones alibuni mfumo wa irabu ambao aliurejejea kama irabu za msingi. Kwa mujibu wa Daniel Jones irabu msingi ni nane kama zinavyoonyeshwa katika kielelezo cha hapa chini.

**Jedwali 3.7 Vokali za Kiswahili**



**Jedwali 3.8 Konsonanti za lugha ya kiswahili**

| Herufi | Fonimu | Neno | Kifonetiki |
|---|---|---|---|
| b | [b] | babu | [babu] |
| ch | [t ʃ] | chama | [t ʃama] |
| d | [d] | dua | [dua] |
| dh | [ð] | dhana | [ðana] |
| f | [f] | fupi | [fupi] |
| gh | [ɣ] | ghali | [ɣali] |
| g | [g] | gogo | [gɔgɔ] |
| h | [h] | hai | [hai] |
| j | [ɟ] | jua | [ɟua] |
| k | [k] | kuku | [kuku] |
| kh | [x] | kheri | [xɛri] |
| l | [l] | leo | [lɛo] |
| m | [m] | mia | [mia] |
| n | [n] | nuru | [nuru] |
| ng' | [ ŋ] | ng'oa | [ŋ ɔa] |
| ny | [ɲ] | nyoka | [ɲ ɔka] |
| p | [p] | pia | [pia] |
| r | [r] | rudi | [rudi] |
| s | [s] | saa | [saa] |
| sh | [ʃ] | shati | [ʃati] |

| | | | |
|---|---|---|---|
| t | [t] | taa | [taa] |
| th | [θ] | thamani | [θamani] |
| u | [u] | ubao | [uba ɔ] |
| v | [v] | vua | [vua] |
| w | [w] | watu | [watu] |
| y | [j] | yai | [jai] |
| z | [z] | zizi | [zizi] |

### 3.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia fonimu za Ekegusii, tumetambua kuwa Ekegusii kina fonimu za irabu na za konsonanti, za vokali ni saba na tano za wakaa, nazo fonimu za konsonanti ni ishirini na moja kwa jumla. Fonimi za Ekegusii ni ishirini na nane. Imedhihirika kuwa fonimu za nusu irabu /w/ na /j/ hazitumiki pekee, huleta maana zinapoandamana na konsonanti zingine.

Kwa mujibu wa Mgullu (1999) Fonimu za Kiswahili zimedhihirika kuwa thelathini na moja. Konsonantini ishirini na sita nazo irabu ni tano. Mfumo wa alama maalum za kifonetiki ambao hutumiwa kuwakilisha foni mbalimbali zilizo katika lugha uliobuniwa na wanafonetiki umeonyeshwa katika jedwali 3.8.

# SURA YA NNE

# TARATIBU ZA UTOHOZI FONOLOJIA

## 4.1 Utangulizi

Katika sehemu hii istilahi za isimu ya Ekegusii (nomino tohozi) zilizokusanywa wakati wa utafiti zimeorodheshwa na kuchunguzwa kisayansi iwapo zimezingatia ufundi wa usayansi. Nadharia ya kisasa na yenye 'usayansi' ambayo imeongoza kazi hii ni nadhari ya istilahi ya kisayansi (NIK). Maana ya 'usayansi katika mbinu ni uwezo wa mbinu za uundaji istilahi za lugha husika kufanyiwa uchunguzi ili kutambua 'ufaafu' wa kila mojawapo, kwa kuzingatia misingi na kanuni za uendelezaji wa leksikoni ya lugha husika Mwaro (2000) Katika sura hii, tumetumia msingi wa utaratibu maalum, utaratibu huu unaeleza kuwa istilahi iundwe kuambatana na utaratibu fulani wa kuunda. Mbinu ya utohoaji imetumika na Abagusii katika kuunda istilahi za isimu ya Ekegusii. Maneno ya Ekegusii yanayotoholewa kutoka lugha ya Kiswahili huchukuwa mikondo tofauti.

## 4.2 Dhana ya istilahi

Kwa mujibu wa Mwaro (2000) Mwangomwango (1977) anaeleza 'istilahi' kama maneno ya kitaaluma ambayo yanatumiwa katika kila taaluma na sharti kila taaluma itengewe maneno kwa ajili ya maelezo maalum. Naye Akida (1975) anaeleza 'istilahi' kwamba ni maneno yanayotumiwa katika sanaa na sayansi. Gibbe (1993) anatumia neno' msamiati' kwa maana moja na 'istilahi' Felber (1984) anasema kwamba istilahi ni ishara ya kiisimu inayowakilisha dhana moja au wakati mwingine dhana nyingine. Tuki (1990) istilahini mfumo wa msamiati maalum unaotumika katika taaluma maalum. Sisi katika tasnifu hii tumetumia neno istilahi kama kisawe cha msamiati kama vile Gibbe (2015).

## 4.3 Maana ya msamiati wa Ekegusii

Msamiati wa isimu ya Ekegusii ni msamiati maalum ulioteuliwa ukapewa umbele, urasmi na kuingizwa katika kamusi ya lughà ya Ekegusii (*Endabasi*). Huu ni msamiati maalum katika taaluma ya isimu unaojidhihirisha katika lugha andishi na katika lugha ya mazungumzo ya kila siku miongoni mwa watumiaji lugha hiyo au kusikiliza katika vyombo vya habari kama vile redio. Hii ndio ilichangia kwa mvuto wetu kukusanya data kutoka redioni (*Egesa fm*).

## 4.4 Isimu

Isimu ni sayansi ya lugha ijishughulishayo na jinsi lugha mbalimbali zilivyopangika na kusikika katika lugha tofauti tofauti ili kufanyiza mfumo wenye misingi yake katika kanuni maalum. Isimu inahusu kanuni zote za lugha na arudhi ambazo ndizo mihimili ya lugha yoyote ile. Isimu ya Ekegusii kama vile na lugha zingine zote ina viwango mbalimbali, viwango hivi ni pamoja na Fonetiki, Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia, na pragmatiki. Tasnifu hii itajikita katika kiwango cha mofolojia na fonolojia.

## 4.5 Maana ya usayansi

Kamusi ya Kiswahili sanifu (1981) sayansi ni elimu inayotokana na uchunguzi, majaribio, vipimo na kudhibitishwa kwa muda uliopo. Nadharia za kisayansi huzingatia kanuni za kijumla au sheria ambazo hujaribu kueleza ni kwa nini jambo au tukio fulani limefanyika. Katika tasnifu hii tutafanyia lugha ya Ekegusii majaribioili 'ufaafu' wake ueleweke. Michakato ya kimofofonolojia inayopitiwa na nomino za Ekegusii wakati wa utohozi inachanganuliwa ili kudhihirisha kuwa nomino tohozi za Ekegusii zinadhibitiwa na kanuni mahususi.

## 4.6 Utohozi Fonimu

Utohozi fonimu unarejelea mageuko ya fonimu za lugha kopeshi (Antilla 1972). Fonimu zisizopatikana katika lugha inayokopa kugeuzwa ili ziafiki kanuni za muundo husika wa kifonolojia. Fonimu zinazobadilishana ni zile ambazo zina uhusiano wa kifonetiki. Kulingana na Mwihaki (1998) baadhi ya fonimu hudumishwa. Fonimu ambazo hudumishwa ni zile zinazofanana kifonetiki. Dhana ya udumishaji humaanisha kwamba kuna fonimu zinazofanana katika lugha kopaji na lugha kopeshi. Fonimu zinachukuliwa kufanana iwapo zina sifa sawa za kifonetiki.

## 4.7 Utohozi wa Konsonanti

Kwa kuwa ni kweli kwamba mbinu ya utohoaji ni 'zalishi' katika kuunda istilahi za lugha, basina utohoaji huo hauna budi kufanywa kwa mfumo maalum na sio kiholela Maneno ya Kiswahili yanapotoholewa mabadiliko hutokea kwa sababu ya tofauti zilizopo kati ya konsonanti za Ekegusii na zile za Kiswahili. Lugha ya Ekegusii haina konsonati zifuatazo:

/d/, / f/, / h//j// l/,/p/,/v/,/x/,/z/, /k/ /c/ /j/, /sh/

Kwa hivyo lugha hii inapokumbana na sauti hizo ngeni huzigeuza na kuzifanya zitamkwe kama zile za Ekegusii. Sifa bainifu mbalimbali hutumiwa kubainisha konsonanti kama zilivyoeleweka na kutumiwa na wanaisimu Jacobson na Halle, na baadaye na wanaisimu Halle na Chomsky. Tutarejelea sifa bainifu zifuatazo katika tasnifu hii:

Ukonsonanti

Namna ya kutamka

Mahali pa kutamkia

**[p] > [ ß]**

Konsonanti za midomo /p/ hubadilikana kuwa kikwaruzo /ß/

| **Kiswahili** | | **Ekegusii** |
|---|---|---|
| /Pete/. | > | /eßete/ |
| /Pipa/ | > | /eßiba/ |
| /Penseli/ | > | /ebensiri/ |

Kipasuo /p/ hugeuka na kuwa kikwaruzo /ß/ kutokana na ukuruba wa kifonetiki unaohusu pahali pa kutamkia. Zote ni konsonanti za midomoni

| p | ß |
|---|---|
| +konsonanto | +konsonanti |
| +kizkwamizo | +kikwamizo |
| +mdomo | +mdomo |

**[z] > [s]**

Kikwaruzo ghuna cha ufizi /z/ hugeuka na kuwa kikwaruzo sighuna /s/

| | | |
|---|---|---|
| /andazi/ | > | [rindasi/ |
| /viazi]/ | > | /eßiasi/ |
| /mwanafunzi/ | > | [omuanafunsi/ |

Fonimu zote hutamkiwa ufizini /z/ na /s/ ni vikwaruzo. /z/ ni sauti ghuna na /s/ ni sauti si ghuna

| /z/ | /s/ |
|---|---|
| +konsonanto | +konsonanti |
| +kikwamizo | + kikwamizo |
| +ufizi | +ufizi |
| +ghuna | -ghuna |

**(i) /f/ > /ß/**

Kikwamizo cha mdomo meno /f /hugeuka na kuwa kikwaruzo cha midomo /ß/

/fulana/ > /eßurana/

/ufunguo/ > /ekeßunguo/

/mfuko/ > /omoßuko/

Mageuko haya husababishwa na sifa za kifonetiki pamoja na jinsi ya kuzitamka.sauti zote mbili ni za midomo na ni vikwamizo

| **/f/** | **>** | **/ß/** |
|---|---|---|
| +konsonanti<br>+kwamizwa<br>+mdomomeno | | +konsonanti<br>+kwamizwa<br>+ mdomo |

**/ɟ/ > /č/**

Mageuko haya husababishwa na sifa za kifonetiki zinazohusu mahali na jinsi ya kutamka fonimu hizi. Sauti zote ni vizuiwa na hutamkiwa kaa kaa gumu tofauti yake ikiwa ni dhamani ya ughuna

| | | |
|---|---|---|
| /maɟibu/ | > | /amačibu/ |
| /maɟi/ | > | /amače:/ |
| /ɟumapili/ | > | /čumapiri:/ |
| /ɟumatano/ | > | /čumatano/ |
| /ɟumatatu/ | > | /čumatato:/ |
| /Iɟ umaa/ | > | /ičuma:/ |
| /kiɟiko/ | > | [egečiko] |

Sauti zote ni vipasuo vya ufizi na sauti zote hutumika katika mazingira ya ndani ya meno.

Kizuiwa ghuna cha kaa kaa gumu / ɟ/ hugeuzwa na kuwa kizuiwa linganifu /č/

**/ ɟ /** > **/č/**

| /ɟ/ | /č/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| + kwamizwa | +kwamizwa |
| +kkgumu | +meno |
| +ghuna | -ghuna |

**/k/** > **/ g/**

Sauti zote hutamkiwa kaakaani

| | | |
|---|---|---|
| /kofia/ | > | /ɛgobi/ |
| /makasi/ | > | /amagasi/ |
| /mkate / | > | /omogati/ |
| /Kiatu/ | > | [/egeato/ |
| /kitambaa:/ | > | /egetamba:/ |
| /kitabu/ | > | /egetabu/ |
| /kitanda/ | > | /egetanda/ |
| /Kikombe/ | > | /egekombe/ |

**/k/** > **/g/**

| | |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kizuiwa | +kikwamizo |

**/ʃ/** > **/s /**

/ʃria/ > [eseria]

/maʃarti/ > [amasariti]

Sauti zote mbili /ʃ/ na /s/ utamkiwa ufisini. Ekegusii haina /ʃ/, s inapokumbana na sauti hii, hutamkwa sawa na ile inayoikaribia /s/

**/v/ > / ß/**

Kikwaruzo cha mdomomeno /v/ hugeuka na kuwa kikwaruzo cha midomoni /ß /. Haya yanasababishwa na sifa za kifonetiki zinazohusu pahali pa kutamkia.

| **Kiswahili** | | **Ekegusii** |
|---|---|---|
| /viati/ | > | /eßiato/ |
| /mwavuli/ | > | /riaßuri/ |
| /mvua/ | > | /emßʉra/ |

| **/v/** | **/ß/** |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kwamizwa |
| +mdomomeno | +mdomo |

**/l/ > /r/**

Konsonanti zote hutamkiwa ufizini na sauti zote ni vilainisho. Konsonanti hizi hushiriki ukuruba wa kifonetiki wa kadiri kubwa.

| | | |
|---|---|---|
| /elfu/ | > | /erißu/ |
| /leso/ | > | /ereso/ |
| /kalamu/ | > | /ekaramu/ |
| /bakuli/ | > | /ebakuri/ |

**/ l/** > /r/

| | | | |
|---|---|---|---|
| +konsonanti | | | +konsonanti |
| +kilainishi | | H | +kilainishi |
| +ufizi | | | +ufizi |

**/th/ ⟶ /t/ au /s/**

Mageuko haya husababishwa na sifa za kifonetiki zinazohusu mahali na jinsi ya kutamka fonimu hizi. Mifano katika nomino ni :

/Themanini/ > /tamanini/

/thelathini/ > /sarasini/

## 4.8 Utohozi vokali

Sifa bainifu za kuainisha irabu za Ekegusii

**a**

+irabu
+mbele
+chini
+mviringo
-ghuna

**ɛ**

+irabu
+kati
-mviringo
-ghuna

**i**

+irabu
+kati
+juu
-mviringo

**u**

+irabu
+nyuma
+juu
+mviringo

**ɔ**

+irabu
+nyuma
+kati
+mviringo

**a:**

+irabu
+kati
+chini
-+mviringo
+urefu

**ɛ:**

+irabu
+mbele
+kati
--mviringo
+urefu

**i:**

+irabu
+mbele
+juu
-mviringo
+urefu

**u** **ɔ**

| u | ɔ |
| --- | --- |
| +irabu | +irabu |
| +nyuma | +nyuma |
| +juu | +kati |
| +mviringo | +mviringo |
| +refu | +refu |

**/i/ > / e/**

Vokali ya juumbele /i/ hujitokeza kama vokali ya kati mbele /e/ katika mazingira fulani.

/kibanda/ > /ekeßanda]/

/kiberiti/ > /ekeßiriti/

/kijiko/ > /egečiko/

/kitamba:/ > /egetamba:/

Mabadiliko haya husababishwa na ukuruba mkubwa wa kifonetiki baina ya vokali hizi kutegemea ulalo wa ulimi. Zote ni sauti za mbele na tena ni sauti tandazi kwa kuangalia uiniko wa ulimi. Vokali /i/ ni vokali ya juu na vokali /e/ ni ya kati juu, kwa hivyo ujirani huu husababisha mageuko hayo.

**(i) /u/ > /o/**

Vokali ya nyuma /u/ hubadilika na kuwa vokali nyuma /o/

/simu/ > /esimi/

/kitunguu/ > / egetunguo/

/chungu/ > /enyongo/

/Nyumba/ > /enyomba/

Mabadiiliko haya husababishwa na ukuruba mkubwa wa kifonetiki baina ya vokali hizi kutegemea uinuko wa ulimi, vokali u ni vokali ya juu ṇa vokali o ni vokali ya kati juu. Zote ni sauti za nyuma.

**/u/ > / i/**

Vokali ya nyuma /u/ hubadilika na kuwa vokali / I/ ya mbele

/simu/ > /esimi/

[sanduku] > /esanduki/

Mabadiliko haya husababishwa na ukuruba mkubwa wa kifonetiki baina ya vokali hizi kutegemea uinuko wa ulimi, zote ni vokali za juu. Vile vile vokali hizi zina uhusiano unaotokana na ulalo wa ulimi, vokali / i/ ni ya mbele na vokali /u/ ni ya nyuma.

/ɔ/ > /i/

Vokali ya nyuma /ɔ/ hubadilika na kuwa vokali ya mbele /i/

/Sindano/ > /esindani/

Mabadiliko haya husababishwa na ukuruba wa kifonetiki baina ya vokali hizi unaotegemea ulalo wa ulimi. Vokali /ɔ/ niya nyuma na vokali /i/ ni ya mbele.

## 4.9 Mofolojia ya Ekegusii

Felber (1984) anadokeza kwamba kuna idadi kubwa ya dhana mpya ambazo huzuka katika nyanja zote za matendo ya binadamu, na ni lazima zielezewe kwa kutumia istilahi zilizoko, ama kuunda istilahi mpya kwa kuambatanisha elementi za neno (mzizi na viambishi) katika lugha husika

Mofolojia ni taaluma inayoshughulikia maumbo ya maneno katika lugha yoyote pamoja na kazi za maumbo yao. Taaluma hii ikishirikiana na taaluma nyingine huangalia jinsi maumbo ya

maneno yanavyoundwa na kazi zake katika lugha (tungo). Katika kuangalia mofolojia ya Ekegusii, tutaangazia uambishi:

### 4.9.1 Uambishaji

Hii ni dhana inayohusu upachikaji wa viambishi kabla au baada ya mzizi wa neno pasipo kubadili kategoria wala kauli ya neno hilo. Kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990) uambishaji, unaelezwa kuwa ni: utaratibu wa kuweka viambishi kwenye mzizi wa neno ili kulipa maana mahususi.

**Jedwali 4.1 Nomino zilizochopekwa vokali 'a'**

| Kiswahli | Ekegusii |
|---|---|
| /maji/ | /amače/ |
| /mavi/ | /amaßi/ |
| / mate/ | /amate/ |
| /mafuta/ | /amaguta/ |
| /makaa/ | /amakara/ |

Abagusii wanapotohoa nomino zisizo hesabika kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Ekegusii kama 1.0 hupata nomino zinazoanza na kiambishi awali cha vokali 'a' silabi tangulizi 'ma' haidondoshwi. Vokali /a/ vilevile hutumika katika kuonyesha kuwa kitu ni kidogo kuliko ukawaida wake, hutumika katika hali ya kudunisha kitu, mfano

**Jedwali 4.1.1 Udogo**

| **Kiswahili** | **Ekegusii** |
|---|---|
| /kijimeza/ | /akamesa/ |
| /kijigari/ | /akagari/ |
| /kijikaratasi/ | /agakaratasi/ |
| /kijisahani/ | /agasani/ |
| /kijisaa/ | /ag:ansa/ |
| /kijikalamu/ | /agakaramu |

**Jedwali 4.2 Nomino zinazochopekwa vokali /o/**

Nomino hizi katika Kiswahili huanza na /m/ kisha konsonanti nyingine inafuata, muundo wa nomino hizi katika silabi ya kwanza ni kkv. Nomino hizi zinapotoholewa na Abagusii huchukua silabi ya kwanza kuwa vokali /o/ kisha inafuatwa na /m/. Muundo unaodhihirika hapa ni vkv.

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| [mlango] | [omorangu] |
| [mwalimu] | [omwarimu] |
| [mchele] | [omočere] |
| [mwaka] | [omwaka] |
| [mti] | [omote] |
| [mwana] | [omwana] |
| [mtu] | [omonto] |

Nomino za kiswahihili zinazoanza na /m/ na za vitu vinavyohesabika zinapotoholewa na Abagusii, nomino hizo huchukua kiambishi awali 'o'. Baada ya kuchopeka /o/ silabi tangulizi /m/ huongezewa vokali 'o' kuunda kiambishi awali 'omo' kisha maendelezi yanabadilika kulingana na fonimu za lugha husika. Tofauti ni wakati silabi ya pili inakuwa kiyeyusho, inapokuwa hivyo neno linabaki vile vile ila litachopekwa vokali'o'mwanzoni.

**Jedwali 4.3nomino zinazochopekwa vokali 'e'**

| kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| /sufuria/ | /esuguri/ |
| /kiɟiko/ | /egečiko/ |
| /kalamu/ | /ekaramu/ |
| /kitaßu/ | /egetaßu/ |
| /nyumßa/ | /enyomßa/ |
| /mßao/ | /eßao/ |
| /kißeriti/ | /ekeßiriti/ |
| /kikomße/ | /egekomße/ |
| /ŋomße/ | /eŋomße/ |
| /sadaka/ | /esataka/ |
| /cho:/ | /echo:/ |
| /kanisa/ | /ekanisa/ |
| /simu/ | /esimi]/ |
| /jiko/ | /ečiko/ |
| /bakuli/ | /ebakuri/ |

| | |
|---|---|
| /sahani/ | /esani/ |
| /kibuyu/ | /ekeßuyu/ |
| /meza/ | /emesa/ |

Nomino hizi zinazochopekwa vokali 'e' ndizo nyingi. Hizi ndizo huchukua muundo asili wa lugha ya Ekegusii. Nomino hizi hutoholewa moja kwa moja bila kubadili silabi zozote, jambo linalodhihirika ni kuwa sauti zisizo katika lugha ya Ekegusii ndizo hubadilika na kuchukua sauti zilizopo katika lugha ya Ekegusii.

### 4.9.2 Uambatishaji

Were (2000) anaeleza kuwa dhana ya uambatishaji katika isimu, ni telezi mno kama inavyodhihirika na kuwepo kwa visawe vifuatavyo vya Kiswahili vyenye kuirejelea:

Maneno pacha, Istilahi za upacha, vikundi jina, vikundi nomino, maneno ungana (Kiingi, 1982)

Mikarabu Gibbe (1981), mwambatano wa maneno (Kapinga, 1975, 1983, 1996), mikarabu (mdee, 1981; Bakita, 1990), kuunganisha maneno (1992), maneno ambatano. Uambatanishaji wa istilahi ni utaratibu ambao unahusu kuteuliwa na kuchukuliwa kwa maneno mawili (au zaidi) yenye maana na yaliyo huru na kuyaunganisha ili kuunda jina moja lenye dhana moja mpya.

Wana isimu na wana lugha wengi kama vile Myachina (1981), Tumbo (1984), Kiango (1984), Mac William (1986), Mwansoko (1989,1990,1993,1996) na Bwenge (1996) wanakubaliana kuwa mbinu ya uambatanishaji ni zalishi, huunda istilahi angavu na zinazoeleweka kwa urahisi na walengwa. Kwa kuwa uambatanishaji huu huunda istilahi angavu, na faafu zinazokubalika kwa walengwa, Abagusii hawakutohoa nomino hizi bali walikuwa na majina yao asilia. Mfano:

**Jedwali 4.4 Nomino ambata**

| **Kiswahili** | **Ekegusii** |
|---|---|
| /Mwananchi/ | - |
| /Kitindamimba/ | Omokogoti |
| /Mwanasheria/ | Omogambi |
| /Mfanyiβiashara/ | Omoonchoreria |
| /Mwekahazina/ | Omogachi |
| /Kinasasauti/ | Rikondo |
| /Kirukanjia/ | Omotayayi |

## 4.10 Hitimisho

Nia ya kuandika sura hii ni kuweka wazi taratibu zilizotumiwa katika utohozi mofolojia na utohozi fonolojia ya Ekegusii. Utohozi huu unasababishwa na sababu kuwa maneno tohozi lazima yaafiki vigezo bayana vya sarufi ya lugha ya Ekegusii. Kipengele cha konsonanti na irabu vimepewa kipaumbele.

Utohozi fonimu ni utaratibu wa kubadilisha sauti bayana za lugha kopeshi na kuzipa muundo wa lugha inayotohoa ili kuafiki sarufi ya lugha hiyo. Hii inasababisha fonimu zisizo katika lugha kopaji kubadilishwa. Utafiti umedhihirisha kuwa vokali zilizobadilika kwa kubadilishana nafasi ni nne. Vokali hizi ni /i/, /o/, /u/, na /ɔ/. Ingawa hakuna hitilafu kubwa baina ya vokali za Ekegusii na za Kiswahili, uhusiano wao wa kifonetiki ulisababisha mabadiliko haya.

Utohozi konsonanti unategemea hitilafu baina ya konsonanti za Ekegusii na zile za Kiswahili. Haya yalisababishwa na sababu kuwa lugha ya Kiswahili ina fonimu zifuatazo ambazo hazipo katika lugha ya Ekegusii:

/p/, /z/, /f/, /sh/, /v/, /l/, /c/, /d/, /h/, /j/

Hivyo Abagusii wanapokumbana na sauti hizi, inabidi wazitamke kwa sauti tofauti lakini inayotamkika kama ile ya Kiswahili.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa katika nomino, konsonanti zote hujitokeza katika mazingira ya kati. Mifano ni kama vile imedhihirika katika sura ya pili (utohozi mofolojia). Katika Ekegusii, konsonanti huungana na viyeyusho. Fromkin na Rodman (1988) wanaeleza kuwa viyeyusho ni sauti ambazo ni nusu irabu na ambazo hutofautiana na irabu kwa kuwa haziundi kilele cha silabi hadi pale zinapowekewa irabu. Lugha ya Ekegusii ina nusu irabu mbili /w/ na//j/ .Mifano ya konsonanti zinazotamkwa pamoja na viyeyusho kama silabi moja:

| | | |
|---|---|---|
| Omwana | /m/ + /w/ | mtoto |
| Enyama | /n/ + /y/ | nyama |
| Enyangi | /n/ +/y/ | harusi |
| Enyamo | /n/ + /y/ | uvimbe |
| Omwaka | /m/ + /w/ | mwaka |

Konsonanti /w/ haitumiki pekee, inaambatishwa na konsonanti zingine. Fonimu /j/ ambayo ni nusu irabu inatofautiana na zingine zote kwa kuwa haijisimamii peke yake. Fonimu hii haitumiki katika maandishi ya Ekegusii bali inatamkwa tu katika maongezi. Utohozi uliongozwa na kanuni na sheria za mofofonolojia ya Ekegusii kupitia sifa mbalimbali za kifonetiki.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.1 Utangulizi

Uchunguzi huu ulifanywa kutekeleza madhumuni ya kuchanganua na kutathmini kanuni za kimofofonolojia zinazotumika katika utohozi wa nomino za Ekegusii kutoka Kiswahili. Nadharia iliyotumika ni ya NIK. Hii ni nadharia ya kisasa inayotazama istilahi za lugha yoyote ile kisayansi. Kwa kuwa isimu ni sayansi ya lugha, nadharia hii ndio itaweka wazi usayansi uliopo. Nadharia ya ukopaji uhamisho pia ilirejelewa kufafanua ikiwa nomino za Ekegusii zilikuwa na majina asilia au nomino zote zilitoholewa. Sura hii inatoa, muhtasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo ya tafiti za baadaye na mahitimisho

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu umebainisha kwamba Abagusii wametohoa nomino nyingi kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Pia imebainika wazi katika utafiti huu kwamba hata kabla ya utohozi, baadhi ya nomino za Ekegusii zilikuwa na majina asilia. Nomino nyingi ambazo zimedhihirika kuwa na majina tohozi ni kwa sababu ni nomino ngeni ambazo zimeibuka kwa sababu ya teknolojia, inabidi maneno hayo yatoholewe ili kukidhi mahitaji mapya yanayozuka. Ni dhahiri kuwa nonimo hizi asilia zilizokuwepo hazina umaarufu wowote kwa wakati huu kwani nomino tohozi ndizo hutumika mno kwa matumizi ya kila siku, sababu hii ndio imechangia kwa vijana kutotumia wala kuelewa maana ya nomino asilia.

Kwa upande mwingine imeonekana kwamba fonolojia na mofolojia zinaungana ili kufanikisha utohozi wa nomino za Kiswahili hadi Ekegusii.Fonolojia ya lugha hizi mbili ililinganishwa na kutambulika kuwa baadhi ya fonimu za lugha hizi zinazoshughulikiwa zinatofautiana. Na hii ndio sababu kuu ya mabadiliko katika maumbo. Uchunguzi huu pia umeshughulikia taratibu za

utohozi mofofonolojia, katika mofolojia mbinu kuu zilizodhihirika ni uchopekaji wa viambishi awali na uambatanishaji. Haya yameweka wazi uelewa kuwa fonimu za lugha ndizo msingi wa uundaji istilahi. Hata hivyo imeonekana katika utafiti huu kwamba kuna mchakato wa ubadala wa konsonanti, katika utohozi konsonanti zinaonekana zikichukua maumbo ya konsonanti za Ekegusii ili kuweza kuafiki muundo mahususi. Zaidi ya haya ni muhimu kutambua kwamba ubadala wa vokali haujaonyesha michakato ya mageuzi mengi kama ilivyodhihirishwa na ubadala wa konsonanti. Hii ni kwa sababu vokali za Ekegusii na Kiswahili zinafanana.

Mbinu za utafiti zilizohusishwa ni pamoja na utafiti maktabani, utafiti nyanjani na usikilizaji wa radio. Utafiti wa maktabani ulifanywa kwa kudurusu vitabu mbalimbali, tasnifu na majarida. Mbinu hii ilikuwa na manufaa katika utafiti huu kwa kuchangia ufahamu wa nadharia zilizotumiwa katika tafiti za awali. Utafiti wa nyanjani ulitufaa mno kwani uasilia wa maneno tohozi ulitambuliwa. Hata hivyo Ekegusii kina wazungumzaji wake asilia katika umri tofauti tofauti. Pia wazungumzaji hao hutumia lugha hii katika shughuli takriban zote za maisha yao.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya NIK na nadharia ya ukopaji uhamisho, uchunguzi zaidi unawezafanywa kutumia nadharia tofauti. Uchunguzi umeonyesha njia tofauti za uundaji istilahi tohozi ambazo ni uchopekaji, uambishaji na uambatanishaji. Kuna njia nyingi za kuunda istilahi ambazo hazikushughulikiwa katika kazi hii, baadhi ya njia hizo ni pamoja na utatizaji, kuunda nomino kutoka kwa kitenzi, nomino kutoka vivumishi, ubunaji, unyambuaji, ufupishaji , akronimu, uhulutishaji na  upanuzi wa maana za maneno. Utafiti zaidi unaweza fanywa kuchunguza kama mbinu hizi zilitumika katika Ekegusii.

Uchunguzi wetu umeshughulikia nomino tohozi pekee. Utafiti unafaa kufanywa kuhusu aina zingine za maneno kama vitenzi, vivumishi, vihisishi, vielezi na viunganishi. Tafiti zote za maneno zitakuwa hazina kubwa kwa tafiti za isimu za lugha za kiafrika.

Istilahi za Ekegusii zilizoshughulikiwa ni zile zilizotoholewa. Utafiti zaidi unahitajika ufanywe pasipo kujikita kwenye maneno tohozi pekee. Isitoshe, Ekegusii hakijatohoa maneno kutoka kwa lugha ya Kiswahili pekee. Utafiti unahitajika ufanywe kudhihirisha kuwa istilahi zimetoholewa hata kutoka kabila zingine kama Kilatini, Kiingereza, Kiarabu na hata kutoka lugha zingine za kibantu.

Kupitia utafiti huu, imebainika kwamba nomino za Ekegusii huchopekwa vokali mwanzoni, hii ni katika hali ya umoja. Kuna nafasi ya uchunguzi kufanywa kwa kuzingatia nomino katika hali ya wingi, nomino hizi katika hali ya wingi zitadhihirisha maumbo tofauti au vipi. Katika utangulizi, tulisema kuwa utohozi hutokea kwa sababu ya mtagusano kati ya watu wa makabila tofauti. Ni kweli kuwa Abagusii wametangamana na Waswahili na maneno haya yakatoholewa. Je, Waswahili nao wametohoa neno lolote kutoka kwa Abagusii? Utafiti huu Unapendekezwa ufanywe. Uandishi wa aina hiyo utawafaidi waandishi wa lugha ya Kiswahili katika kujumuisha lugha zilizochangia katika uundaji wa istilahi za Kiswahili.

## 5.4 Hitimisho

Katika kuhitimisha ni bayana kwamba katika utafiti huu, nomino tohozi za Ekegusii zimeweza kutambuliwa, michakato ya kimofofonolojia kudhihirishwa na kanuni za kimofofonolojia zinazoongoza utohozi huu kuweza kubainishwa. Hivyo utafiti huu umeweza kutimiza malengo yaliyodhamiriwa katika utafiti huu.

## MAREJELEO


Anderson, B. (1972). *Contributions to Generative Phonology* University of Texas Press: Austin London.

Antilla, R. (1972). *An Introduction to History and Comparative* Linguistics New York: Macmillan.

Bosire, B. M. (1993). Ekegusii: "A Comparative study of Rogoro and Maate Dialects**".** Tasnifu Isiyochapishwa ya MA. Chuo kikuu cha Nairobi.

Crystal, D. (1991). *A Dictionary of Lingustics and Phonetics* New York: Blucked Publisher.

Gesare, (1992). "Mofolojia ya Lugha ya Ekegusii" Tasnifu haijachapishwa ya MA. Chuo kikuu cha Nairobi.

Guthre, M. (1947). Comparative Bantu. An Introduction to Comparative Linguistics and PreHistory of Bantu Languages

Gregg: Farnborough.__M__(1948*) Classification of Bantu Languages*. Oxford University Press Gromova (2008)

Haugen, E. (1990). "Analysis of Linguistic borrowing". Washington: George Town University.

Hooper, J. B. (1976. *An Introduction to natural generative Phonology*.Academic Press.

Houpe, D. W. (1978). "Loan words in Baraza: A Study of Lexical Otigins in Kiswahili Language Newspapers", PHD Thesis University of Carolina.

Habwe, J. and Karanja, P. (2004*). Msingi wa Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi Phoenix publishers.

Irebe Mwangi, P. (2008). "A Sychronic Segmental Morphology of Standard Swahili" Unpublished PHD Thesis' University of Nairobi

Lass, R. (1984). Phonology: An introduction to basic concepts. Cambridge University Press.Retrieved from https:// books.Google dot com/books.

,yons, J. (1968). *Introduction to theoretical linguistics* New York: Cambridge University press.

/lassamba, D. P. B. Kihore, Y. M. Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar-es-salaam: Tuki.

/lbaabu, I. (1985). New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research and Literature. Nairobi: Kenya literature Burea.

/lgullu, R. S (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi Longhorn publisher

/lills, G. E. na Gay, L. R (1992) Educational research: competencies for analysis and applications. Pearson

/logaka, R. (2009) "Fonolojia ya utohozi wa maneno mkopo ya Ekegusii kutoka Kiswahili". Tasnifu isiyochapishwa ya MA. Chuo Kikuu cha Kenyata.

Mohamed, M. (2001). *Modern Swahili Grammer*. Nairobi: sunlit Ltd.

Mugenda, O.M and Mugenda, A.G (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches:* Nairobi: Act press.

Mwaliwa, C. H (2000). "Ulinganishi wa Mofofolojia ya Kiswahili na Kidawida". Tasnifu haijachapishwa ya MA Chuo kikuu cha Nairobi.

Mwaro, A.G (2000). "Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili". Tasnifu ya Uzamifu.chuo kikuu cha Egerton, Kenya

Ngowa, N. J. (2015). "Uchanganuzi wa Nomino-mkopo za Kirinyaga Kutoka Kiingeresa". Tasnifu isiyochapishwa ya MA Chuo kikuu cha Nairobi.

Nyakundi (2010). "Motivational Morpho Phonological processes in Egesembesa Argot AmongEkegusii- Speaking Males of Western Kenya". Tasnifu isiyochapishwa ya MA. Chuo Kikuu cha Kenyata.

Obawa (2012). "Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha Ya Ekegusii" Tasnifu isiyochapishwa ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Obwoge, C. K. B. (2014). " A Lexico Semantic analysis of Ekegusii circumcision social variety", Tasnifu ya M.A. University of South Africa.

Osinde, K. N. (1988). " A morphosyntactic Analysis of Ekegusii". Unpublished M.A. Thesis University of Nairobi.

Otiende (2013). "Athari za Kimofofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu Kama Lugha ya Pili". Tasnifu isiyochapiswa ya MA. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ochichi (2013). "Usimbaji Maana Kimazumgumzo katika Ekegusii". Tasnifu isiyochapishwa ya MA. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Robert Elwel. Ekegusii Verb Morphology.

Tuki (ed.) (2006). *Tuki English-Swahili Dictionary: Kamusi ya Kiingeresa Kiswahili (3rd ed)* Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Waithaka, N.M. (2010). "Mofolojia ya Maneno Mkopo ya Gikuyu kutoka Kiswahili". Tasnifu isiyochapishwa ya M. A Chuo Kikuu cha Kenyata.

Whitelly, W. H. (1963). *Loan-words in Kamba*: A preliminary Survey; African Language Studies, *4 146. 165*

Whitelly, W. H. (1956). *A Practical Introduction to Gusii.* Nairobi: East African Litrature Bureau.

## KIAMBATISHO

## SAYANSI NA TEKNOLOJIA

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Ratili | Eratiri |
| Randa | Eranda |
| Simu | Esimi |
| Sindano | Esindani |
| Saa | Ensa |
| Makasi | Amagasi |
| Ufunguo | Ekebunguo |
| Pesa | Chibesa |
| Gari | Egari |

## MSAMIATI WA KIMASOMO

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Mwanafunzi | Omwanafunzi |
| Kalamu | Ekeramu |
| Kitabu | Egetabu |
| Sanduku | Esanduku |
| Mfuko | Omoguko |
| Meza | Emesa |

| | |
|---|---|
| Mlango | Omorangu |
| Karatasi | Ekaratasi |

## MSAMIATI WA JIKONI

| **Kiswahili** | **Ekegusii** |
|---|---|
| Kikombe | Egekombe |
| Kijiko | Egechiko |
| Kiberiti | Ekebiriti |
| Sahani | Esani |
| Chungu | Enyongo |
| Bakuli | Ebakuri |
| Kibuyu | Ekebuyu |
| Jiko | Echiko |

## MSAMIATI WA MAVAZI NA MAPAMBO

| **Kiswahili** | **Ekegusii** |
|---|---|
| Suruali | Esuruari |
| Kofia | Egobia |
| Sidiria | Egesindereo |
| Buibui | Ebuibui |
| Kirinda | Amarinda |

| | |
|---|---|
| Kabuti | Ekabuti |
| Kitenge | Egetenge |
| Kanzu | Ekansu |
| Pete | Ebete |

## MSAMIATI WA DINI

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Sadaka | Esataka |
| Kanisa | Ekanisa |
| Korani | Ekorani |
| Yesu | Yeso |
| Sala | Esara |
| Madhabahu | - |

## MSAMIATI WA WANYAMA

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Punda | Ebunda |
| Ng'ombe | Engombe |
| Farasi | Ebarasi |
| Simba | Esimba |
| Chui | Echui |

| | |
|---|---|
| Mbuni | Embuni |
| Twiga | Etwiga |
| Ngamia | Engamia |
| Nyuni | Enyoni |

## MSAMIATI WA VYAKULA

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Munyu | Omonyo |
| Chumvi | Echumbi |
| Kitunguu | Egetunguo |
| Viazi | Ebiasi |
| Mchele | Omochere |

## MSAMIATI WA SIKU ZA WIKI

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Jumapili | Chumabiri |
| Jumatatu | Chumatato |
| Jumatano | Chumatano |
| Alhamisi | Aramisi |
| Ijumaa | Ichuma |
| Jumamosi | Chumamosi |

## MSAMIATI WA MAJIRA NA NYAKATI

| **Kiswahili** | **Ekegusii** |
|---|---|
| Kiangazi | Omorakera |
| Leo | Rero |
| Magharibi | Mogoroba |
| Juma | Echuma |
| Mwaka | Omwaka |

## MSAMIATI WA SEHEMU ZA MWILI

| **Kiswahili** | **Ekegusii** |
|---|---|
| Kichwa | Omotwe |
| Nywele | Etukia |
| Sikio | Ogoto |
| Shavu | Emboto |
| Ulimi | Oromeme |
| Titi | Orobere |

## MSAMIATI WA HISABATI

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Ishirini | Isirini |
| Thelathini | Sarasini |
| Arobaini | Arobaini |
| Hamsini | Amisini |
| Sitini | Oisitini |
| Sabini | Sabiini |
| Themanini | Tamanini |
| Tisini | Tisaini |
| Mia | Emia |
| Elfu | Eeribu |
| Milioni | Emirioni |

## NOMINO AMBATA

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Mwananchi | Omwanainchi |
| Mfanyabiashara | Omonyabiasara |
| Mwanakijiji | Omwanakijiji |
| Mwanasiasa | Omonyasisasa |